

# **UFAFANUZI WA KANUNI NA MAISHA YA NDUGU WA KIUME NA WA KIKE WA UTAWA HASA WA TATU WA MTAKATIFU FRANSISKO**

## **HISTORIA**

Katika karne XIII, wengi walivutiwa na karama ya Mt. Fransisko wa Asizi, lakini hawakutaka au hakuweza kujiunga na Ndugu Wadogo au na Mabibi Fukara. Hivyo wakafanya toba ulimwenguni, wakiishi nyumbani kwao au upwekeni; mapema baadhi yao waliunda jumuia ili kuishi pamoja na kutoa huduma mbalimbali.

Lakini katazo la Mtaguso IV wa Laterano (1215) lilizua wasipewe kanuni maalumu mpaka mwaka 1289 ambapo Papa Mfransisko Nikola IV akawatungia (kwa jina la "Memorale Propositi" = "Ukumbusho wa Azimio"). Hata hivyo kanuni hiyo haikutofautisha Watersyari walioishi ulimwenguni (Wasekulari) na walioishi kijumuia (Waregulari).

Mwaka 1521 Leo X akatoa kanuni mpya kwa hawa wa mwisho akiwaita Tertius Ordo Regularis (T.O.R.) yaani Utawa Hasa wa Tatoo wa Mt. Fransisko.

Mwaka 1927 Pius XI akatunga kanuni mpya tena, lakini haikuwa na roho ya Kifransisko, ila sheria tu za kufanana na zile za watawa wowote.

Hata hivyo karama ya Kifransisko ilizidi kuenea na kupochezwa kwa vizazi na nchi mpya.

Katika Mtaguso II wa Vatikano (1962 1965) Kanisa lote likaja kujitambua linahitaji hali mpya ukahimiza mashirika yote yajirekebishe upya hasa kwa kurudia chemchemi ya Ukristo na karama ya mwanzilishi. Agizo lilidai watawa wote wahuishwe, nao wakachangamkia utekelezaji, ingawa kwa nia tofauti sana. Kabla yake hakuna kizazi kilichopewa jukumu na idhini ya namna hiyo.

Kutokana na maendeleo ya teolojia, mwanga wa Mtaguso, upatikanaji na uchimbaji wa chemchemi za Kikristo na za Kifransisko, urahisi wa mawasiliano, na hasa msukumo wa Roho Mtakatifu, umati wa TOR (mashirika 387 ya kike yenye jumla ya masista 200,000, pamoja na mashirika 27 ya kieme yenye jumla ya ndugu 20,000) ukaweza kuchangia utungaji wa kanuni mpya ambayo iwaunganishe wote bila ya kufuta tofauti zao nydingi (kuhusu asili, malengo, jinsia, mazingira n.k.).

Polepole ushirikiano uliongezeka, hasa katika mikutano mikuu ya mwaka 1976, 1979 na 1982. Katikati iliundwa kamati ya kimataifa ambayo ilikuwa na wajumbe wa mabara yote na kupokea majibu kutoka nchi 30, kwa lugha 10, kutoka mashirika 205 na wengineo. Kutokana na mchango huo muswada wa kanuni uliacha kufuata sana ile ya Ndugu Wadogo ya mwaka 1223 ukachota zaidi katika ile ya mwaka 1221 (zaidi ya nusu ya madondoo yote uliyonayo) na katika Himizo kwa Ndugu wa Toba.

Mkutano mkuu wa mwisho uliupitia na kuupiga kura muswada huo para kwa para, halafu jumla, ukiwa na sura 9 na para 32, na kutumia maneno ya Mt. Fransisko karibu peke yake.

Dibaji, inayotumia nusu ya kwanza ya Himizo kwa Ndugu wa Toba la Mt. Fransisko, inaunganisha kanuni mpya na asili ya utawa. Sentensi ya kwanza na baraka ya mwisho ni kama katika kanuni ya mwaka 1927, na hivyo zinaonyesha mlolongo wa historia. Masharti muhimu ya zamani yalizingatiwa pamoja na utambuzi wa karama halisi kadiri ya mwanzilishi na ya mapokeo.

Kazi hiyo yote ilikabidhiwa kwa Mama Kanisa na hatimaye tarehe 8-12-1982 Yohane Paulo II aliipitisha kwa hati "Franciscanum Vitae Propositum" akisisitiza upekee wake.

Kadiri ya kanuni mpya tunu ya msingi ya utawa huo, yaani toba ya kudumu, inazaa maisha ya sala, ufukara na unyenyekevu katika mazingira ya kidugu.

Kanuni inaleta uhai mpya, ule wa maneno yaliyo roho na uhai, ikituweka kati ya maziara ya zamani na mipango ya milenia mpya. Kuikubali kwa pamoja kunatuunganisha Waregulari wote katika hatua mpya ya hija yetu duniani, ingawa kila shirika linahitaji katiba maalumu ili kuamua namna ya kutekeleza roho hiyo ya Kifransisko katika nafasi mbalimbali sana.

Lengo la kanuni ni hasa kutuelekeza tushike maneno, maisha, mafundisho na Injili takatifu ya Bwana wetu Yesu Kristo kwa kuongoka mfululizo, kama alivyotaka mzee wetu Fransisko.

## **KICHWA**

**Kanuni na maisha...** Karama ya mzee wetu Fransisko na ya Watersyari wa kwanza, kisha kujaribiwa na maisha na kuthibitishwa na mamlaka ya Kanisa imekuwa kanuni ambayo iongoze mashirika yote ya Utawa Hasa wa Tatoo na kila ndugu ndani yake. Kwa kuthibitisha kanuni yoyote, Kanisa linawahakikishia waamini kuwa hiyo ni njia nyofu ya utakatifu.

Karama yoyote inapopata kanuni inakuwa na muundo unaokusudiwa kuidumisha. Kwa kuwa kanuni inadai itekelezwe: kila mmoja anapaswa kuitekeleza, ndiyo sababu ana pia haki ya kusaidiwa na jamaa yake kuitekeleza; vilevile jamaa inapaswa kumsaidia kila ndugu aitekeleze, hivyo ina haki ya kumdai aishike kanuni hiyo.

**... ya Ndugu...** Kwanza tunaitwa Ndugu ili tufungamane kwa upendo na wote na vyote. Ni jina la Kiinjili kwa kuwa Yesu aliwaita hivyo mitume wake (Math 28:10) na watu wowote (Math 25:40) akasema, "Nyinyo nyote ni ndugu" (Math 23:8). Kwa msingi huo Mt. Fransisko alidai viongozi pia waitwe ndugu kama wenzao.

Udugu unadai usawa na upendo, tena mkubwa kuliko ule wa mama yeote kwa mwanae aliyemzaa kimwili, kwa kuwa udugu huo mpya ni wa Kiroho, na roho ni bora kuliko mwili. Hata hilo lina msingi katika Injili, Yesu alipowaita ndugu zake hasa wanaotimiza matakwa ya Baba (Mk 2:35).

Umoja wa Wafransisko wa kwanza, waliokuwa watu wa kila aina, ulikuwa ushuhuda bora wa kuwa wanamfuata Kristo (Yoh 13:34-35). Umuhimu wa jambo hilo ulisisitizwa na Mt. Fransisko hasa katika Wasia Mfupi wa Siena, ambamo, kabla hajawadai ndugu zake washike ufukara na Ukatoliki aliwadai wapendane daima kama mwenyewe alivyofanya.

**... wa Kiume na wa Kike...** Utawa wa Tatu ni kwa jinsia zote mbili. Hata mashirika ya utawa huo zamani yaliweza kuwa na nyumba za kiume na za kike chini ya mkuu mmoja. Kitu hicho baadaye kikapingwa na kwisha, lakini siku hizi kinawezekana tena kutokana na upana wa mawazo wa sheria mpya za Kanisa.

**... wa Utawa Hasa wa Tatu wa Mtakatifu Fransisko.** Utawa huo ulianza wakati alipoishi mzee wetu, kwa kuwa, mbali na wale walioshika maisha ya toba nyumbani mwao, wengine walianza kukusanyika pamoja ili kuishi kitawa karibu na konventi za Ndugu Wadogo au kwingine, hata upwekeni.

Wafransisko hao wakaja kuitwa Utawa wa Tatu, kwa kuwa wengi wao walikuwa walei, si makleri wala watawa hasa. Baadaye jina hilo likaja kuelewaka tofauti, kama aina ya tatu ya Wafransisko, baada ya Ndugu Wadogo (I) na Mabibi Fukara (II).

Kuanzia karne XV walioshika mashauri ya Kiinjili waliitwa Utawa Hasa wa Tatu (T.O.R.), ambao leo ni mkuubwa kuliko mwingine wowote wa Kanisa, hasa baada ya mashirika mengi kuanzishwa karne mbili za mwisho.

Wafransisko wote wanaunda familia moja tu: tofauti kati yao ni mikazo mbalimbali katika karama ileile na utume ueleule.

### **MANENO YA MTAKATIFU FRANSISKO KWA WAFAASI WAKE**

Yamechukuliwa kutoka Himizo kwa Ndugu wa Toba (I,1-9). Hayohayo (na yaliyoyafuata) yapo pia mwanzoni mwa kanuni ya Wafransisko Wasekulari. Hiyo inaonyesha wazi kwamba mzizi wao na wetu ni mmoja, yaani tapo la toba lililomtangulia Mt. Fransisko miaka 600 hivi.

Watubu waliwajibika kuongoka mfululizo kwa matendo ya binafsi na ya hadhara ya sala na malipizi: baadhi waliendelea kuishi ulimwenguni, baadhi walikwenda upwekeni, au kwenye kanisa au monasteri fulani bila ya kujifunga kama watawa.

Mwanzoni mwa uongofu wake Mt. Fransisko pia alifanya hivyo akitafuta njia yake. Ndiyo sababu yeye na wafuasi wake wa kwanza walijiita Watubu wa Asizi kabla ya kuchagua jina la Ndugu Wadogo.

Walipokubaliwa na Inosenti III kuwa shirika (1209), waliacha kuwa Watubu wakawa watawa hasa. Hata hivyo wakaendelea kuwaathiri na kuwashughulikia Watubu wengi, ambao Mt. Fransisko aliwaandikia Himizo katika matoleo mawili: la kwanza ni la kabla ya mwaka 1215.

Nusu yake ya kwanza ndiyo iliyopangwa mwanzoni mwa kanuni hii ili kutukumbusha maelekezo ya mzee wetu na uhusiano wetu naye, ingawa kanuni nzima imetungwa kwa kutumia sanasana maneno aliyoyaandika katika nafasi nyingine.

### **SURA YA KWANZA**

#### **KWA JINA LA BWANA! HUU NDIO MWANZO WA KANUNI NA MAISHA YA NDUGU WA KIUME NA WA KIKE WA UTAWA HASA WA TATU WA MTAKATIFU FRANSISKO.**

Kufuatana na maneno ya Mtume Paulo (Kol 3:17), Mt. Fransisko alifanya yote kwa jina la Bwana. Kwa namna ya pekee katika kazi kubwa ya kuandika kanuni alikuwa na hakika ya kuongozwa naye. Maneno hayo aliyoyatumia yeye kuanzia kanuni yametumika humu pia.

Kwa jumla sura ya kwanza inachora kiini cha karama tuliyoshirikishwa na Mt. Fransisko na Ndugu wa Toba waliotutangulia. Karama hiyo kwetu ni kanuni ambayo iongoze maisha yetu ya kidugu hata watu wote waweze kuitambua ndani mwetu.

### **PARA YA 1°**

Para hii inasema kwa ufupi kuwa mtindo wa maisha yetu ni kumfuata Yesu kitawa kwa kuzingatia hasa Injili kwa mfano wa mzee wetu Fransisko aliyetuelekeza tujikane na kujitahidi sana tushike sio tu amri bali pia mashauri ya Bwana.

**Mtindo wa maisha wa Ndugu wa Kiume na wa Kike wa Utawa Hasa wa Tatu wa Mtakatifu**

**Fransisko ndio huu: kufuata Injili takatifu ya Bwana wetu Yesu Kristo...** Ubora wa kanuni unategemea jinsi inavyolingana na Injili. Kanuni nyingine za kitawa zinafuata mwongozo wa Kiinjili. Kumbe Mt. Fransisko alichagua Injili yenye we iwe kanuni yake, akatudai tuishike moja kwa moja.

Wazo hilo, pamoja na wazo la Ukatoliki, linasisitizwa mwanzoni na mwishoni mwa kanuni, kama Alfa na Omega ya maisha yetu. Mengine yote yaliyoandikwa katikati yanategemea na kutekeleza hayo mawili.

Mt. Fransisko hakuandika kanuni ishike nafasi ya Injili bali iyapigie mstari mambo kadhaa ya Injili ili kuwasaidia wafiasi wake waitekeleze kikamilifu. Lakini hakutaka turidhike na kushika yale tu yaliyomo katika kanuni; hivyo kwa makusudi mazima alitaja mwanzoni na mwishoni wajibu wa kushika Injili ili ashinde upinzani wa waliotaka wapunguziwe masharti yake. Hakukubali kufanya walivyomtaka, akijua wito wake ndio kuambatana kabisa na Bwana wake, akitafakari mfululizo maneno na matendo yake na kutafuta daima namna ya kuishi kama yeye, pamoja naye na ndani yake. Kwa hiyo hadi kufani aliwasitisizia ndugu zake kwamba washike Injili kuliko sheria nyingine yoyote, kwa kuwa ndiyo walivamuahidia Mungu moja kwa moja.

Huo upendo wa Fransisko kwa Injili ni mamoja na hamu yake ya kurudia maisha ya Yesu hapa duniani, ambayo yalimtambulisha Mungu alivyo, na kwa hiyo hayawezi kupita kamwe, bali yanapima na kuhukumu maisha yoyote ya binadamu kizazi hata kizazi.

Yesu anatuambia, "Mkinipenda, mtashika amri zangu... Anayepokea amri zangu na kuzishika ndiye anayenipenda...Mkishika amri zangu mtadumu katika upendo wangu" (Yoh 14:15-21; 15:10). Basi, kutohana na upendo tulio nao kwake, na kwa lengo la kufikia upendo mkubwa zaidi, tuwajibike kushika sio tu amri za Yesu bali Injili yake nzima.

Uaminifu huo unaleta ujuzi wa pekee wa ukweli unaotufanya huru: "Mkishika neno langu mtakuwa wanafunzi wangu kwelikweli, mtajua ukweli, nao ukweli utawafanya huru" (Yoh 18:31-32).

Hasa ni kung'amua zaidi upendo wa Mungu kwa kustawisha urafiki wa dhati na Yesu: "Anayenipenda atapendwa na Baba yangu, nami nitampenda na kujidhihirisha kwake... Nyinyi ni rafiki zangu mkifanya ninayowaamuru" (Yoh 14:21; 15:14).

Matunda ya kufuata matendo ya Yesu, hasa kujishusha kwa upendo, ni kupata heri na uwezo wa pekee juu ya moyo wa Mungu: "Mkijua hayo, mtakuwa heri mkiyatimiza... Ikiwa maneno yangu yanadumu ndani yenu, ombeni lolote nanyi mtapewa" (Yoh 13:17; 15:7).

Basi, tukifuata njia hiyo tutaelewa zaidi na zaidi ubora wake, uliomfanya Mt. Fransisko akatae katakata kanuni nyingine yoyote, nasi tutafanana na mtu mwenye busara aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba (Math 7:24-27).

**... kwa kuishi kwa utiifu, kwa ufukara na kwa useja mtakatifu.** Katika kufuata mtindo wa Injili takatifu Mt. Fransisko alishika kwa nguvu zake zote hayo masharti matatu ambayo kwa pamoja ndiyo kiini cha aina yoyote ya maisha yaliyowekwa wakfu katika utawa. Kwa kuyataja mwanzoni mwa kanuni, mara baada ya Injili, alionyesha wazi kuwa Ndugu Wadogo (na vilevile sisi) si walei wanaofanya toba, bali ni watawa hasa, ingawa wa aina mpya.

Kushika hayo matatu ni kuchagua ufuasi wa Yesu kama mpango wa maisha yote. Mtaguso II wa Vatikano umesema kuwa mtawa, ili amfuate kwa karibu zaidi na kuambatana naye kabisa, anayapokea hayo mashauri yanayoitwa ya Kiinjili kwa kuwa yanapatikana katika mafundisho na hasa katika maisha ya Yesu. Hayapokei kwa sababu za kibinadamu, bali kwa ajili ya Yesu tu; hayapokei ili kujipatia maadili bora tu, bali ampate Yesu mwenyewe.

Hayo mashauri matatu yanatuwezesha kulinganisha maisha yetu na yale alijojichagulia Bwanaarusi wetu. Yote matatu yanatuvutia kutohana na upendo na hamu moja, nayo yanachangia utekelezaji wake: kuishi pamoja na Yesu, kama alivyoishi yeye.

Kwake hayo matatu yalikuwa misimamo ilijoja roho na maisha yake, tunavyoona hasa katika mafumbo yake makuu; vilevile kwa mtawa hayo ni misimamo ya kudumu ambayo ashiriki kazi ya wokovu ya Yesu hata kufa pamoja naye.

Mtawa akishiriki kikamilifu maisha na kifo cha Bwana, anashiriki pia utukufu wake, akionyesha tayari mwanzo wa uzima wa milele na sura yake kama Adamu mpya.

Kwa kifupi maisha yaliyowekwa wakfu kwa mashauri ya Kiinjili yanamtegemea kabisa yeye, katika maisha yake duniani na katika ufufuko wake. Baada ya kifodini tu, ndiyo namna bora ya kumpenda na kumfuata.

Kuanzia mwishoni mwa karne ya XII mashauri hayo matatu yalisisitizwa kama mambo makuu ya utawa, kiasi kwamba wengine wakauona huo ni kuweka nadhiri tatu. Mt. Fransisko aliyapokea hayo matatu ila hakusema juu ya nadhiri, wala hakuyatenganisha na ufuasi wa Injili nzima. Hatimaye Mtaguso II wa Vatikano ukayarudisha mashauri hayo katika nafasi yake halisi, kama njia za kufikia kwa urahisi zaidi ule upendo kamili kwa Mungu na kwa jirani ambao ndio lengo lenyewe.

Kwa Wakristo wote ndiyo amri kuu tulioachiwa na Yesu; katika kuitekeleza mtawa anaafuata njia ya mkato ya mashauri ya Kiinjili, wakati wengine wanafuata njia mbalimbali za kawaada ili kuufikia utakatifu huo wanaoitiwa wote. Ingawa Mkristo halazimiki kufuata njia fulani, tunapaswa kupokea na kutangaza mafundisho rasmi ya Kanisa ya kwamba utakatifu unachangiwa kwa namna ya pekee na mashauri ya Bwana, ambayo ni mengi, lakini hayo matatu ndiyo muhimu zaidi.

Mtawa akiyahidi anaondoa vipingamizi vinavyoweza kumzuia asitekeleze kikamilifu amri kuu ya upendo.

Bila ya shaka, akitekeleza hayo mashauri asitekeleze amri hiyo ni bure kabisa, kwa kuwa mashauri ni njia, si lengo.

Katika Kanisa maisha yaliyowekwa wakfu ni yale ambayo Mkristo anapokea rasmi mashauri hayo matatu katika mtindo wa kudumu uliokubalika. Hayo matatu yanaendana kama ilivyokuwa kwa Yesu mwenywewe: yote yanatokana na upendo unaojitoa na kulenga upendo mkuu kabisa.

Kwa upendo huo mtawa anakubali kujinyima mambo mema yanayostahili heshima, yaani kutumia jinsia katika ndoa ili kujenga familia, kushughulikia mali anavyopenda, kujipangia mahali na namna ya kuishi: hayo yote si madhambi wala mambo ya kudharauliwa ambayo tuyakwepe. Tena kujinyima hayo ni hasara fulani inayoumiza: ndiyo sababu Yesu alitoa mfano wa towashi, yaani mwanamume mpungufu kijinsia.

Mtawa anaamua kwa hiari kumfuata Yesu katika njia hiyo ya kujishusha hata kufa kwa utiifu; basi, kama vile Yesu aliviyotukuzwa kwa kufanya hivyo, hata mtawa anayemfuata kwa karibu zaidi anashiriki uzima wake mpya katika Roho Mtakatifu, akijiona huru zaidi katika upendo na kuwa kielelezo katika utukufu wa useja, ufukara na utiifu wake.

Bila ya shaka, utekelezaji wa mashauri hayo unashiriki daima fumbo la Pasaka: unatufanya tufie mfululizo umimi wetu ili tuishi kwa upendo kamili zaidi na zaidi. Hivyo unadai uongofu au toba ya kudumu.

Kati ya mashauri hayo matatu lile kuu ni utiifu, ambao tunamtolea Mungu matakwa yetu, kwa kuwa hayo ni tunu na sadaka kubwa kuliko mwili na moyo ambayo inatolewa kwa useja, na kuliko vitu vingine vinavyotolewa kwa ufukara. Hasa ni kuu kwa kuwa ndio kiini cha msimamo wa Mwana wa Mungu: ni kwa kumtii Baba kwamba alishika ufukara na useja atoe utumishi bora. Ndiyo sababu kanuni inataja utiifu kabla ya mashauri mengine.

Utawa wowote unapaswa kushika yote matatu, lakini kila mmojawapo unayashika kulingana na karama yake maalumu. Hivyo kuna tofauti kati ya mashirika kuhusu namna ya kushika mashauri ya Kiinjili. Tofauti kuhusu useja haiwezi kuwa kubwa au haipo kabisa, kumbe ipo kuhusu utiifu na zaidi kuhusu ufukara. Hiyo inatokana na neno lenyewe ufukara ambalo linaweza kuwa na maana mbalimbali, njema na hata mbaya; pia kipimo chake kinaweza kuwa tofauti kulingana na watu wanaoitwa fukara katika mazingira wanamoishi.

Mt. Fransisko alitofautisha shirika lake na mengine kwa kulidai lishike ufukara mkuu ambao kwake ni sawa na kuishi bila ya mali ya binafsi wala ya shirika, pamoja na kulenga upande wa roho kutoambatana na tunu yoyote ya kibinadamu tu. Kwa kufanya hivyo alisogea mbali na mapokeo ya kimonaki na kurudia mtindo wa Injili takatifu. Mapinduzi hayo yalikaribia kusababisha utawa wake usikubaliwe au ukafutwe baadaye. Pia yakaleta migogoro mingi shirikani. Lakini yeye na Mt. Klara hawakurudi nyuma hata kidogo katika jambo hilo la pekee la karama yao; halafu historia ya shirika ikaonyesha wazi ubora wa msimamo huo.

**Wanaomfuata Yesu Kristo kwa mfano wa mtakatifu Fransisko...** Kwa mara nyingine kanuni inasisitiza tumfuate Yesu, ila katika kufanya hivyo tunatakiwa kuzingatia mfano aliotuachia Mt. Fransisko: ndiyo namna yetu maalumu ya kumfuata Yesu.

**... wanatakiwa kufanya mengi zaidi na makubwa zaidi...** Maneno hayo na yale yanayofuata yamechukuliwa kutoka Himizo kwa Ndugu wa Toba (II,36-40) ambamo Mt. Fransisko anatueleza sababu ya sisi kupaswa kufanya mengi na makubwa kuliko Wakristo wenzetu: kwa kuwa tumeacha ulimwengu na mappingamizi yake, tuna jambo moja tu la kufanya, yaani kumpendeza Bwana pekee bila ya mgawanyiko wa moyo.

Humohumo tunaambiwa pia tusizingatie tu yaliyo maalumu ya utawa, kiasi cha kusahau yanayotupasa kama waamini wote. Ndivyo ilivyowatokea Mafarisayo kadiri ya lawama ya Yesu kwamba, walishika vipengele vidogovidogo na kuyaacha mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na imani (Math 23:23). Ndivyo ilivyotokea mara nyingi mashirikani, watawa waliposhika mapokeo yao kuliko Injili na amri kuu ya upendo, mpaka ukaja Mtaguso II wa Vatikano kuwashtua ukidai Injili ihesabiwe kuwa kanuni kuu ya utawa wowote.

**... kwa kushika amri na mashauri ya Bwana wetu Yesu Kristo...** Mt. Fransisko alijua na kutaja wazi tofauti kati ya amri za Mungu na mashauri ya Kiinjili, akatuhimiza kuvishika vyote kwa kuwa vimetoka kwa Bwana wetu.

**... na wanapaswa kujikana kama kila mmoja alivyomuahidia Mungu.** Tunapaswa kujikana hasa kwa kutii, anavyozidi kutuambia Mt. Fransisko katika Himizo hilo: ndiyo sababu anatukumbusha kuwa ndivyo tulivyomuahidia Mungu, mbali ya kwamba ni sharti la kumfuata Yesu (Math 16:24), aliyekuwa mtiifu hata kufa, naam, hata kufa msalabani.

## **PARA YA 2°**

Para hii inasisitiza toba kama kiini cha karama ya Utawa wa Tatoo katika familia ya Kifransisko, ambacho kinazaa sala, ufukara na unyenyekevu. Inakazia vilevile kuwa kazi hiyo ya kumuongokea Mungu haina mwisho duniani, bali inadai izidi kufanyika. Ili tushike Injili kiaminifu tunapaswa kutubu mfululizo kama alivyofanya mzee wetu Fransisko, ambaye maneno yake yanayotumika humu yametoka Kanuni ya Muda

(21:9; 23:4-7).

**Ndugu wa kiume na wa kike wa utawa huu...** Mt. Fransisko aliongeza, "watumwa wasio na faida" (Lk 17:10), neno la Injili alilolipenda sana kwa kuwa lilimsaidia kukumbuka na kushika ukweli wa hali yetu mbele ya Mungu.

**... pamoja na wale wote wanaotaka kumtumikia Bwana Mungu ndani ya Kanisa takatifu, katoliki la mitume...** Ndilo taifa la watu waliopatanishwa na Mungu kwa njia ya toba; ndipo tunapozidi kutubu kwa msaada wa wenzetu, hasa waandamizi wa Mitume waliopewa uwezo wa kuondolea dhambi. Ni Kanisa takatifu kimsingi, lakini linahitaji daima utakaso na urekebioso kutokana na ukosefu wa viungo vyake.

Mzee wetu alipenda daima kuwashirikisha wote yale aliyojaliwa na Mungu, hasa maisha ya kumtumikia kwa sala na toba. Ndiyo maana aliongeza orodha ndefu ya Wakristo wanaoalikwa kutubu: "mapadri, mashemasi, mashemasi wadogo, maakoliti, wapungapepo, wasomaji, mabawabu na makleri wote, watawa wote wa kiume na wa kike, watubu na vijana wote, mafukara na wenye shida, wafalme wakubwa kwa wadogo, wafanyakazi na wakulima, watumishi na mabwana, mabikira, waseja na wake wote, walei wote wa kiume na wa kike, watoto, wenye kubalehe, vijana na wazee wote, wazima kwa wagonjwa, wadogo kwa wakubwa pia, mataifa, rangi, makabila na lugha zote, nchi zote na mataifa yote popote duniani, waliopo na watakaokuwepo". Yaani wote, wote, wote kabisa.

**... wadumu katika imani na toba za kweli.** Mt. Fransisko aliongeza sababu ya kufanya hivyo: "la sivo hakuna atakayeokoka". Uzima wa milele unategemea imani ya kweli, sahihi kadiri ya mafundisho ya Kanisa hilo. Lakini imani bila ya matendo imekufa, haiwezi kuokoa tena. Halafu Yesu alisisitiza, na Fransisko vilevile, kwamba ni lazima tudumu mpaka mwisho ili tuokoke. Mtu akishika jembe halafu anaangalia nyuma hafai kwa utawala wa Mungu (Lk 9:62).

**Wanataka kuishi uongofu huo wa Kiinjili...** Ndilo lengo la kuingia utawani, kuzidi kuipokea Injili katika mawazo, maneno na matendo yetu ili yalingane na yale ya Yesu na hivyo tufanane na Baba yetu wa mbinguni aliye mkamilifu.

**... kwa roho ya sala, ya ufukara na ya unyenyekevu.** Sura za kanuni zinazofuata zitaeleza kinaganaga jinsi toba inavyofanyika kwa hayo, kadiri ya karama ya Kifransisko.

**Basi, wajiepushe na ovu lolote...** Upande wa kwanza wa toba ni kuachana na maovu yoyote. Mt. Fransisko aliyahi kuongeza, "na yenye sura ya uovu". Tukumbuke juhudzi zake katika kushinda vishawishi na kukwepa makwazo.

**... na kudumu mpaka mwisho katika uadilifu...** Hayo pia ni maneno yake ambayo alitaka wafuasi wake wote wawewe kuyatumia ili wawahimiza watu watubu. Ndio upande wa pili wa toba: kutenda mema, kuzaa matunda. Maana haitoshi kukwepa dhambi tusipotekeleza upendo kwa matendo na ukweli, tena mpaka mwisho.

**... kwa kuwa Mwana wa Mungu mwenyewe atakuja kwa utukufu...** Atakuja kuhukumu, akibagua kondoo na mbuzi. Labda tunasita kukubali maneno ya Mt. Fransisko ambayo kwa kirefu yanasesma, "Tunakushukuru kwa kuwa Mwanao mwenyewe atarudi katika utukufu wa enzi yake kuwapeleka katika moto wa milele walialaaniwa ambao hawakufanya toba wala kukufahamu..." Ndio utulivu wa mwanasala anayeridhika na kazi zote za Mungu, mwenye haki na huruma zisizo na mipaka. Lakini kabla ya siku hiyo tunapaswa kufanya juu chini ili wote tutubu kweli. Kwa ajili hiyo Mt. Fransisko alitaka ndugu zake wahubiri hasa juu ya "vilema na maadili, adhabu na utukufu" (Kanuni ya Kudumu 9:3).

**... na kuwaambia wale wote waliomfahamu na kumuabudu na kumtumikia katika toba...** Kadiri ya mzee wetu toba ndiyo njia ya kutimiza lengo la Muumba, kwamba tumfahamu, tumuabudu na kumtumikia kwa upendo.

**"Njooni, mliobarikiwa na Baba yangu, mrithi ufalme mlioandaliwa tangu mwanzo wa ulimwengu".** Mt. Fransisko alitumia maneno hayo ya Yesu yanayowaelekewa waliowatendea kwa huruma wadogo wake wenye shida, njaa, kiu n.k. Hivyo tunakumbushwa kwamba toba inalenga upendo na kwamba sadaka pamoja na sala na mfungo ndiyo njia yake kuu. Tangu mwanzo Ndugu wa Toba walitoa huduma nyingi katika jamii.

### **PARA YA 3°**

Para hii inaanza kwa kupanua maneno ya ile ya pili kuhusu imani sahihi na Ukatoliki, ikidai uaminifu kwa Kanisa na kwa mchungaji wake mkuu. Umoja huo ndio msingi wa umoja ndani ya kila shirika na kati ya

Wafransisko wote.

**Ndugu wa kiume na wa kike wanaahidi kuwa na utiifu na heshima kwa Papa...** Kanuni imerithi maneno ya namna hiyo kwa Mt. Fransisko aliyeyatuma kufuatana na mtindo ulioenea Ulaya karne za kati, kwanza katika utawala wa siasa, halafu katika Kanisa pia: kwamba mdogo alikuwa anapiga magotia mbele ya mkubwa na kumuahidia utiifu na heshima. Ndivyo mzee wetu alivyomfanyia Inosenti III (1209) kwa niaba ya waandamizi wao pia: hivyo kwa mara ya kwanza utawa fulani kwa jumla ulifungamana kabisa na Papa ukiwa tayari kumtii katika yote na kutumwa naye kufanya kazi yoyote. Basi, Ndugu Wadogo wakawa jeshi la amani la Papa kwa urekebishiwa Kanisa kadiri ya Mtaguso IV wa Laterano.

Upande wa Mt. Fransisko ahadi hiyo ilitokana na upendo wake kwa mtume Petro na waandamizi wake, na imani yake katika Kanisa la Roma. Ndiyo sababu, tofauti na wazushi, alinua kabisa kushika Injili akifuata kikamilifu uongozi wa Kanisa hilo. Kwake hakuna upinzani kati ya Injili na Kanisa, karama na muundo, unabii na utiifu.

Kwa kutudai tuwe moja kwa moja chini ya Papa alituelekeza njia ya kuzaa matunda mengi kwa ufalme wa Mungu, badala ya kudhani sisi tu tumeelewa Injili au tumeangaziwa na Mungu hata tukadharau msimamo wa Kanisa. Mt. Fransisko alitaka hivyo wakati Ulaya ilipojaa uzushi, ndiyo sababu liturujia inasifu Ukatoliki wake.

Kila mfuasi wake anapaswa kujaa upendo kwa mama yake, Kanisa takatifia la Roma na kulitegemeza kama alivyoota Inosenti III. Tunapaswa kuishi na kukua Kikanisa chini ya mkuu wa maaskofu, tukifua kwa bidii mafundisho, maagizo na miongozo yake, hasa yanapopingwa na wengi.

**... na kwa Kanisa Katoliki.** Yaani kwa Kanisa lote chini ya wachungaji wake, na kwa Kanisa maalumu (yaani jimbo) chini ya askofu wake. Hatuwezi kudai eti, tunamfuata Papa, huku tukishindana na maaskofu wenzake. Ili kukwepa hatari hiyo, Mt. Fransisko alitukataza tusimkimbilie Papa ili kupewa naye idhini za pekee kinyume cha matakwa ya maaskofu, kwa mfano kwa ajili ya utume. Zaidi ya hayo alitaka kuwatii hata mapadri duni katika madaraka yao.

**Kwa roho hiyohiyo wawatii waliowekwa kuihudumia jamaa.** Katika Kanisa, kila jumuia na shirika linahitaji vilevile miundo na uongozi. Kwa kutii wahudumu tunazidi kulijenga Kanisa katika umoja. Basi, baada ya Mt. Fransisko kumuahidia Inosenti III utiifu na heshima, wenzake walimuahidia vilevile yeye na waandamizi wake. Hivyo, kwa njia ya mtumishi wake, shirika lote limeunganika chini ya Papa, imara katika imani na umoja.

Tofauti na mapokeo ya kimonaki, ambapo kila monasteri inajitegemea na watawa hawaihami, Wafransisko, ambao wanatawanyika popote duniani ili kuishi na kwenda kwa utume, wanazidi kuwa jamaa moja kwa kuwa chini ya mtumishi mmoja. Mamlaka yake inashirikiwa kwa kiasi chao na wahudumu wengine na washauri, ambao tunapaswa kuwatii vilevile.

**Halafu, popote wanapokaa...** Yaani katika nyumba wanamoishi.

**... na popote watakapokutana...** Yaani katika kwenda ulimwenguni kwa utume wao, hata wasipofahamiana kwanza.

**... watakiwe kupokeana...** Ni maneno ya Kanuni ya Muda (7:15) kama yale yanayofuata: upendo na udugu unaotunganisha unadai tumpokee kila mmoja jinsi alivyo kama Mungu anavyotupokea sisi.

**... na kuheshimiana Kiroho na kwa bidii.** Pamoja na kuwaheshimu viongozi wa Kanisa na wa shirika, tunapaswa kumheshimu kila mmoja si kiroho tu, bali kwa matendo, hasa akiwa na shida. Upendo wa kidugu utufanye tutambue shida hizo hata kabla hazijatajwa na tujitolee kadiri ya uwezo wetu.

**Pia wastawishe umoja na ushirika na viungo vyote vya familia ya Kifransisko.** Watoto wote wa Mt. Fransisko wanaunda familia moja tu: viongozi wa matawi matatu ya Utawa wa Kwanza, ambao wana mamlaka juu ya Waklara wengi pia (yaani Utawa wa pili), na viongozi wa T.O.R., wa Baraza la Kimataifa la Kifransisko (mashirika ya Utawa wa Tatu) na wa Wafransisko Wasekulari kwa pamoja wameunda Baraza la Familia ya Kifransisko. Tunapaswa kustawisha na kulinda umoja huo tulioufikia baada ya karne nyingi za mashindano ya bure na kijicho.

Katika familia hiyo moja kuna nafasi kwa karama mbalimbali au mikazo tofauti, mradi tusivuruge udugu ambao ni sifa kuu ya kwanza ya kila Mfransisko halisi.

### **SURA YA PILI NAMNA YA KUPOKEA MAISHA HAYA**

Kama vile katika kanuni za Mt. Fransisko na Mt. Klara, sura ya kwanza imeweka misingi ya maisha yetu; kabla sura nyingine hazijaeleza zaidi maisha yenye, hii ya pili inafafanua namna ya kuingizwa katika

mtindo wetu wa kuishi, ambao ni tofauti kabisa na ule uliozoleka ulimwenguni.

Hivyo sura hii inazingatia malezi, ambayo ni ya kudumu kama vile toba inayotupasa (para 6). Katika mapokeo yetu toba inajitokeza katika ufukara (para 5), utumishi mnyenyekemu (para 7) na sala (para 8) ambayo imepangwa mwishoni mwa sura ili kutuingiza katika ile inayoizungumzia kwa kirefu. Kuanzia hapa tunu hizo nne za msingi zinajitokeza katika kila sura ya kanuni.

Para hizo zinategemea sana mang'amuza ya Fransisko katika kuongoka na kulea wafiasi wake, pamoja na mkazo wa Kanisa la leo juu ya haja ya malezi sio tu wakati wa kuingia utawani, bali maisha yetu yote.

#### **PARA YA 4°**

Para hii fupi inazungumzia miito na mapokezi yao kufuatana na maneno ya Kanuni ya Muda (2:1-2) na ya Kanuni ya Kudumu (2:1).

**Wale wanaofika kwetu...** Zamani za Mt. Fransisko na hata baadaye kwa karne nyingi, miito ilikuwa inajiotea, tena kwa wingi, kutohana na mvuto wa maisha na mahubiri ya watawa. Kumbe siku hizi Kanisa linatuhimiza tuitafute kutohana na uhaba wa wafanyakazi katika shamba la Bwana. Hata hivyo Yesu ametufundisha kuwa njia bora ni kuiomba.

**... kwa mwanga wa Bwana...** Mzee wetu alitambua kidole cha Mungu katika uongofu wake na katika wito wa wenzake. Hivyo alidai katika suala la wito kila mmoja aongozwe na mwanga huo, asifuate sababu za kibinadamu (k.mf. kujihakikishia riziki). Unahitajika utambuzi ambao inafaa ufanyike kwa msaada wa kiongozi wa kiroho. Wafransisko wenyewe wanaweza kutoa msaada huo.

**... wakiwa na nia ya kupokea maisha haya, wapokewe kwa wema.** Tofauti na mapokeo ya Kibenedikto, yaliyotaka nia za watu wa namna hiyo zijaribiwe na wamomaki kwa ukali siku za kwanza, Mt. Fransisko alidai wapokewe kwa wema. Ni kwamba yeche aliona kwa imani kila wito ni zawadi ya Mungu kwa mtu mwenyewe na kwa shirika (Wasia 14 unasema, "Bwana alinijalia ndugu"), zawadi ambayo ipokewe kwa furaha.

**Halafu wakati wa kufaa watambulishwe kwa watumishi wenyewe mamlaka ya kuingiza katika jamaa.** Yaani mapokezi yafuate sheria za shirika husika, kwa kupiga hatua baada ya hatua hadi kuwa na wajibu na haki zote kama ndugu wengine. Mamlaka ya kuwapokea rasmi si ya wote, bali ni ya baadhi ya viongozi kadiri ya sheria.

#### **PARA YA 5°**

Para hii inahusu uchambuzi wa miito unaofanyika sambamba na malezi ya Kiinjili. Kwa mara nyingine yanatumika maneno ya Kanuni ya Kudumu (2:2; 2:5).

**Watumishi wahakikishe...** Kwa kuwa wana mamlaka ya kupokea na ya kukataa waliofika, wanapaswa kuwachunguza ili waone kama kweli wana wito toka kwa Mungu. Mt. Fransisko alidai huo tu, badala ya kutaja masharti mengi kuhusu akili, elimu n.k. Uchunguzi huo unafanyika hasa kwa kujadiliana nao ili kutambua pamoja matakwa ya Mungu.

**... kuwa watakaji wanashika kweli imani katoliki na sakramenti za Kanisa.** Ndilo jambo la msingi kabisa, kwa kuwa maisha yote yanategemea imani. Masharti mengine yamerekebishesharekebishesha na Kanisa, lakini hilo lipo hata leo kwa mashirika yote.

**Wakiwa wanafaa waingizwe katika maisha ya jamaa.** Kanuni inachora malezi kama kuingizwa katika maisha ya jamaa, yaani kung'amua na kuzoea maisha hayo badala ya yale ya ulimwenguni: badiliko hilo linachukua muda mrefu likitaka kuwa la dhati, tena linafanyika hatua kwa hatua.

Kati yake Kanisa linakazia kwa namna ya pekee umuhimu wa unovisi, kwa kuwa limeng'amua kwamba "ustawi wa mashirika unategemea hasa jinsi wanavyochanguliwa na kulelewa" (Paulo VI). Ndiyo sababu siku hizi linakataza mtu asipokewe kuanza unovisi kabla hajaandaliwa vya kutosha, hasa kiroho.

**Basi, wafafanuliwe kwa makini...** Mang'amuza tu hayatoshi pasipo maelezo na mafundisho ya makini, kwa kuwa binadamu anaongozwa na akili, nayo inataka kujua sababu za kutenda namna fulani. Mpango wake una tofauti kadiri ya shirika, ingawa baadhi ya mambo yanaagizwa na Kanisa kwa watawa wote.

**... yote yanayohusu maisha haya ya Kiinjili...** Kadiri ya imani ya Mt. Fransisko, maisha yetu yanafuata hasa Injili, hivyo katika malezi yetu ndiyo kitabu kikuu, ingawa si pekee.

**... hasa maneno haya ya Bwana...** Yaani yale ambayo mwanzoni mwa jamaa Fransisko na wenzake waliyasoma katika Injili, walipofungua Misale mara tatu ili kujua matakwa ya Mungu.

**"Ukitaka kuwa mkamilifu, nenda ukauze vyote ulivyo navyo ukawape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni, kisha njoo unifuate".** Zamani za Mt. Fransisko, maneno hayo ya Math 19:21 yalitamkwa na mtumishi kwa mtakaji kabla hajaanza unovisi: lilikuwa jaribio la kwanza la nia yake, na sharti la kuweza kumfuata Yesu fukara. Siku hizi Kanisa limelahirisha hadi wakati wa kuweka ahadi ya daima, ili kuepuka hatari ya mtu kubaki shirikani kwa sababu tu ulimwenguni hana tena mbele wala nyuma.

Hata hivyo malezi ni safari ya kubandukana na yote ili kuambatana na Yesu. Ni ajabu kuona mtu anaingia utawani hana kitu, halafu anazidi kujilimbikizia: atafikaje ukamilifu kwa kufuata uroho badala ya kutekeleza upendo kwa maskini na kujivekea akiba mbinguni?

**Na, "Mtu akitaka kunifuata, ajikane nafsi yake ajitwike msalaba wake na kunifuata".** Kuachana na mali hakutoshi; maneno hayo ya Yesu (Math 16:24) yanaonyesha kuwa ufuasi wake unatudai tujikane mpaka ndani na kupokea msalaba "kila siku" (Lk 9:23). Hivyo tu tunaweza kujitoa kabisa kwa Mungu pamoja na Mwanae mpenzi.

#### **PARA YA 6°**

Para hii ni kati ya zile zinazotuhusu moja kwa moja, si katika hatua za kuingizwa utawani tu, bali hata baada ya miaka mingi, kwa kuwa Mt. Fransisko aliona tunapaswa daima kuanza upya maisha ya toba. Nayo hayaishii hewani, bali yanahusisha mwili wetu na kujitokeza katika mavazi na mengineyo.

**Hivyo, kwa uongozi wa Mungu, waanze maisha ya toba...** Si kwa kujipangia, bali kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu, ambaye anajua kuliko sisi tunahitaji marekebisho yapi.

**... wakijua ya kuwa wote tunapaswa kuongoka mfululizo.** Zaidi na zaidi, hasa kwa kuzidi kujifanya watoto mbele ya Mungu (Mt 18:3).

**Kama alama ya uongofu...** Mt. Fransisko hakuridhika na nadharia isiyogusa maisha, bali alidai daima matendo yatokeze yaliyomo moyoni. Hivyo alipenda kudhihirisha kwa alama mbalimbali maana ya mtindo wake wa ajabu. K.mf. alipenda kucaa kanzu yenye sura ya msalaba ili ionyeshe lengo la maisha yake.

Kwa kuzingatia masharti ya Yesu kwa Mitume alipowapeleka mara ya kwanza, Mt. Fransisko alitaka kuonekana ametumwa na Bwana: kuwa si tu mtu anayeishi toba na ufukara, bali pia mtu wa Kanisa anayefanya utume ili kuokoa watu; tena anafanya utume kulingana na wito wake wa udogo.

Sura ya nje ya Mfransisko inatakiwa kuzingatia Injili na kutokeza ufukara, unyenyekevu na toba. Kulegeza masharti katika mavazi kunaharibu hata maisha ya kiroho na ya kitume, kwa kuwa mavazi yenye ni kinga dhidi ya mitindo ya dunia na dhidi ya vishawishi mbalimbali, nayo yanahubiri ubatili wa malimwengu na hivyo yanachangia utume wa kuhubiri toba kwa matendo na maneno.

**... na ya kuwekwa wakfu kwa maisha ya Kinjili...** Kanisa hasa leo, katika utamaduni wa picha, linasitiza umuhimu wa mavazi ya kitawa kama ushuhuda wa hadhara wa kujitoa kwa Mungu na wa kushika ufukara. Ndivyo liliyofanya katika Mtaguso II wa Vatikano (PC ) na katika Mkusanyo wa Sheria za Kanisa (CIC ). Kwa namna ya pekee Wafransisko, wakiwa watiifu kwa Kanisa na wafuasi wa ufukara mkuu, wanapaswa kucaa kitawa bila ya aibu.

**... wavae nguo duni...** Zilingane na wito wa udogo na ufukara. Yesu mwenyewe alidai ziwe chache sana, akasema wanaovaa mavazi maridadi, mahali pao ni katika nyumba za wafalme. Kanuni ya Ndugu Wadogo inafafanua idadi ya nguo zao na kuruhusu kuzitia viraka vya gunia na vitambaa vingine.

**... na kuishi pasipo makuu.** Wangkuwa wanafiki kama wangevaa kifukara, kumbe nyumba na mtindo wa maisha kwa jumla vingekuwa vya fahari. Usahili wa maisha ya Yesu unatakiwa kung'aa katika yale ya Wafransisko, hasa wakati mwenyewe unaendelea kuonja njaa katika umati wa akina Lazaro. Kumuongokea kunadai tumhurumie na kwenda kinyume cha mikondo ya ulimwengu, unaofuata kiburi na tamaa.

#### **PARA YA 7°**

Para hii inazungumzia kilele cha safari ya malezi, yaani ahadi ya daima, na misimamo inayohitajika katika maisha ya toba ya kudumu. Maneno hayo yamo katika Kanuni ya Kudumu (2:11).

**Halafu, muda wa jaribio ukishamalizika...** Zamani za Mt. Fransisko jaribio lilichukua mwaka mmoja tu, kumbe siku hizi ni miaka kadhaa, kadiri ya sheria za Kanisa na za shirika husika. Hata kama mtu ameweka ahadi ya muda, jaribio linaendelea upande wake na upande wa shirika.

**... wapokewe kwenye utiifu...** Tofauti na wamonaki waliojifunga kudumu katika monasteri fulani, Wafransisko wanapokewa kwenye utiifu, yaani wanaweza wakaishi popote duniani, kadiri watakavyotumwa,

lakini kwa kudumisha uhusiano na ndugu wengine kupitia viongozi wao na kwa kushika pamoja nao imani na misimamo ya maisha.

**... wakiahidi kushika daima maisha haya na kanuni.** Zamani za Mt. Fransisko kulikuwa na aina moja tu ya "professio": neno hilo la Kilatini maana yake ni tamko la hadhara kuhusu imani uliyonayo au kazi ya kudumu unayoifanya. Mtu anapoifunga kuishi kitawa anatoa "professio" yake.

Siku hizi ziko za aina mbalimbali, kulingana na sheria za Kanisa na za shirika husika: kuu na ndogo, ya muda na ya daima, yenyenadhiri au vifungo vingine.

Kanuni yetu haitaji kamwe nadhiri, ila hapa tunasikia neno "kuahidi", linalotufanya tujiulize: kumuahidia nani? Mungu au watu? Kwa kuwa neno hilo ndilo lilitotumiwa na Mt. Fransisko, ni lazima kulielewa kama alivyofanya mwenyewe.

Alipoandika Kanuni ya Kudumu (1223) Kanisa tangu miaka mitatu lilikuwa likisisitiza kuwa professio ya Ndugu Wadogo ni "nadheri". Hivyo hao wakaanza kutamka kwamba wanamuahidia kushika kanuni Mwenyezi Mungu, halafu mwaka 1260 wakaongeza kuwa wanamwekeea nadhiri ili iwe wazi zaidi. Kwa namna hiyo Kanisa lililinganisha ahadi yao na ya watawa wengine zilivyoolezwa karne hiyo hiyo.

Leo Katekisimu ya Kanisa Katoliki inatofautisha kidogo ahadi kwa Mungu na nadhiri, na hivyo inafungua njia ya kurudia mtindo uliokuwepo Mt. Fransisko alipokuwa hai. Kwa vyovoyote tofauti kati ya ahadi kwa Mungu na nadhiri ni ya kisheria tu.

Ahadi kwa Mungu (au nadhiri) ni jambo zito sana linalodai kushikwa kutokana na adili la ibada na ambalo likivunja ni sawa na kuvunja amri ya kwanza ya Mungu hata kutenda dhambi ya mauti. Upande mwingine, kwa nadhiri vitendo vyema vinakuwa ibada kwa Mungu na kustahili zaidi tuzo lake. Anayetimiza nadhiri anajitao kwa Mungu kuliko mtu anayetenda yaleyale pasipo nadhiri. Tena, kwa nadhiri utashi unaimarika kutenda mema, na hivyo maadili yanakamilika, kama vile kutenda dhambi mfululizo kwa makusudi kunazidisha uovu wa tendo baya.

Suala lingine zito ni kwamba tunamwekeea Mungu ahadi ya kushika kanuni au nadhiri zile tatu tu. Jibu la kanuni ni wazi, ikitumia tena maneno ya Mt. Fransisko, inaeleza kuwa ahadi ni ya kushika maisha na kanuni yetu. Tamko hilo linasisitiza umoja wa sadaka ambayo tunamtolea Mungu, yaani maisha yetu yote jumla yakifuata kanuni nzima, sio tu mambo matatu yasiyohusiana utiifu, ufukara na useja. Kwa tamko hilo si hayo matatu tu, bali pia mengine yaliyomo katika kanuni yanapata kuwa na uzito wa adili la ibada k.mf. kushika udogo, kupendana kidugu, kulitii Kanisa, kuvumilia matatizo n.k. La sivyo kanuni ingebaki tu sheria ambayo haihusiki sana na nadhiri, yaani na agano la kindoa kati yetu na Mungu.

Kumbe tukiahidi kanuni nzima tutafanya yote yaliyomo ili kuitikia kwa upendo wetu upendo wa Mungu aliotuita tuishi vile, na ili kumtukuza kwa adili la ibada tukitekeleza ahadi. Tutekeleza kanuni kwa kuwa tumemuahidia Mungu kufanya hivyo kama ibada ya upendo, sio kwa sababu ni sheria ya shirika tu. Hivyo kila neno la kanuni lina nguvu kubwa zaidi ya kutakasa sisi na kumtukuza Mungu.

Tarajio ni kwamba kila mmoja aisikie hamu ya kutoa ahadi hiyo moja kwa moja, kwa siku zote za maisha yake. Katika mashirika ya kitawa Kanisa linamda hiyo nadhiri ya daima itanguliwe na miaka mitatu au zaidi ya nadhiri za muda ili kuhakikisha msimamo. Lakini ili nadhiri ya muda iwe halisi si batili ni lazima mtawa awe na nia ya kufikia hatua ya kuweka ile ya daima. Kwa vyovoyote mkazo ni upande wa ahadi ya daima ambayo hasa inafanana na ndoa isiyovunjika na inamweka wakfu mtu. Kama vile katika ndoa, maisha yanayofuata yanaweza yakawa marefu na ya shida, lakini mtawa anatakiwa kusimama imara kwa kushika kiaminifu ahadi aliyoitoa kwa hiari.

Kudumu katika wito aliojaliwa na Mungu ni jambo muhimu sana kwa kila mmoja. Daima Kanisa limejitalidi kuhakikisha kuwa walioifunga mbele ya watu kuishi kitawa wasirudi nyuma. Ingawa siku hizi sheria zake zinaeleza uwezekano wa kuliacha shirika, zinadai sababu nzito na ruhusa ya viongozi wa Kanisa au pengine wa shirika.

Kudumu hivyo ni neema ya Mungu inayopatikana kwa sala na kwa juhudzi za kutekeleza kila siku vizuri zaidi ahadi yetu. Kwa kawaida mtawa mwenye bidii haachi wito wake. Kumbe kushindwa ni tokeo la makosa mengi madogomadogo bila ya kujitahidi kujirekebisha. Hivyo katazo la kanuni la kuacha shirika linadai pia uaminifu katika yote, Ndugu asije akashindwa kudumu utawani.

**Basi wakiweka pemberi hangaiko na fadhaiko lolote** Kutiundolea hayo ni kazi ya ufukara mtakatifu ambao tunajiachia mikononi mwa Mungu Baba yetu mwema. Ni ukombozi wa moyo wetu unaowezesha \neno la Mungu kuzaa kwa wingi maishani mwetu, mara thelathini, sitini had mia, alivyonukumbusha mzee wetu.

**Wajitahidi kwa kila namna kumtumikia, kumpenda, kumheshimu na kumuabudu Bwana Mungu** Ndio lengo la maisha yetu ambalo Mt. Fransisko alitukazia, yaani kuishi kwa ajili ya Mungu, kwa kuwa ndicho anachotaka kuliko yote.

**Kwa moyo safi na akili safi** Ndiyo namna ya kuishi hivyo kadiri ya Mt. Fransisko. Ibada kwa Mungu inafanyika kwa usafi wa moyo na wa akili. Basi, neno hilo linalohusika sana na useja mtakatifu, unaofanya moyo uwe wa Mungu tu pasipo mgawanyiko, linakuja kufuata neno la utiifu na neno la ufukara, hayo matatu

yanatuelekeza kufanya imara agano letu la Mungu na yanatuingiza katika para ya 8 inayohusu sala katika maisha ya toba na inayoandaa vema sura ya tatu inayoeleza kwa kirefu maisha yetu ya sala.

**8.** Para hii inakaza baadhi ya maneno na mawazo ya Mt. Fransisko ambayo kilele chake ni kutambua ukweli wa kwamba sisi ni makao ya Utatu Mtakatifu.

**Watengeneze daima ndani mwao maskani na makao** Mt. Fransisko akikumbuka daima agizo alilopewa na Msulubiwa huko San Damiano, la kutengeneza upya nyumbe yake, aliona kuwa halikuhusu tu jingo lile, bali Kanisa hai na kila roho ndani yake. Hivyo kwa maneno hayo yanayofuata yale ya para ya 7 katika Kanuni ya Muda 22 26 27, anatuhimiza sisi pia kutekeleza agizo hilo ndani mwetu ili Mungu afanye maskani yake humo kama Yesu alivyoahidi. Tujitahidi daima kufanya roho yetu iwe safi ili impendeze anayetaka kukaa ndani yake.

**Kwake ye ye aliye Bwana Mungu mwenye enzi, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu** Mt. Fransisko alizama ndani ya fumbo hilo la Utatu, hivi kwamba kila mahali anaonyesha kuwa maisha yake ya kiroho yalitegemea uhusiano wa dhati na nafsi hizo tatu. Lengo letu pia ni hilohilo, si lingine lolote, kuungana na Baba ndani ya Kristo kwa njia ya Roho.

**Ili wakue kwa miyo isiyogaanyika** Kumpenda kweli Mungu kuliko yote na wote, si nusunusu tu, ndiyo faida inayokusudiwa katika utawa.

**Katika upendo kwa wote** Kujaa uhai na upendo wa Mungu kunastawisha upendo kwa jirani yoyote na kujitokeza kwa matendo ya upendo wa kidugu. Ndiyo matunda halisi ya toba aliydai Mt. Fransisko tuyazae, na ndiyo mapokeo ya Utawa wa Tatu.

**Wakiwageukia mfululizo Mungu na jirani** Uongofu weu wa mfululizo ndio huo, ni kuelekea upya kwa Mungu na kwa jirani, badala ya kujipendelea.

### **SURA YA TATU ROHO YA SALA**

Kanuni katika sura ya kwanza imeeleza wazi msingi wa maisha yetu, yaani kuishi Injili katika Kanisa. Katika sura ya pili imeeleza jinsi utawa unavyoenea na unavyojitokeza na tabia maalumu ya nje na ya ndani. Katika sura ya tatu inaanza kueleza kinaganaga maisha yenyewe yanayoongozwa na upendo kuelekea utakatifu. Kwa kuwa upendo unamueleke kwanza Mungu, kanuni inaeleza kwanza maisha ya sala alivyofanya Mt. Fransisko mwenyewe.

Sala inashika nafasi ya kwanza katika wito wa watawa wote, na hasa sisi ambao katika sura zinazofuata tunakumbushwa mfululizo ukweli huo. Ni kwa sababu wengi wanakimbilia utendaji hata kumsahau Yule amabaye ndiye lengo pekee la utendaji wote, Yule ambaye ni mpenzi mkuu wa roho zetu, Yule ambaye pekee yake anatuwezesha kuzaa matunda ya kudumu. Mtawa anaitwa kuwa mtaalamu wa muungano na Mungu, lakini asipojifanya upya katika sala siku kwa siku, anamezwa na ulimwengu na kupotewa na maana ya wito wake.

Kutoka kwenye himizo la kujifanya maskani ya Utawa Mtakatifu tunaingia kwenye kuhtasari wa tabia kuu za sala ya Kifransisko. Mzee wetu hakuacha mbinu maalumu za kusali kama walivyofanya baadhi ya watakatifu, lakini ametuaelekeza sna kuungana na Mungu Utatu Mtakatifu. Daima sala yetu imuelekee Baba kwa njia ya Mwana kwa nguvu ya Roho Mtakatifu na izingatie kazi za Mungu kwa ajili yetu, hasa Umwilisho wa Mwanae, kwa ajili hiyo tumtolee mfululizo sifa na shukrani kwa maneno na matendo.

**9.** Para hii inatokana kwa kiasi kikubwa na sura za mwisho za Kanuni ya Muda 22 29 30, 23 8 11, hivyo imejaa eoho na maneno ya Mt. Fransisko ambaye tunachochewa nayo sana. Ujumbe ni kwamba kwetu sala ni namna maalumu ya kuishi, si jambo la wakati Fulani tu. Ibibujike kutoka ndani mwetu moja kwa moja, bila ya sisi kukata tamaa kamwe, kwa kuwa Baba anataka tuwe kitu kimoja naye. Ndio utakatifu tulioitiwa, ndiyo ibada yetu halisi kwake.

**Popote, kila mahali, kila saa na kila wakati** Ndiyo sababu sura hii kichwa chake ni Roho ya sala haina mipaka. Kila mahali na kila saa na kila hali ya nje na ya ndani inafaa kwa sala.

**Ndugu wa Kiume na Kike wamuamini kweli na kwa unyenyekevu** Roho ya sala ni roho ya imani inayotambua daima uwepo na utendaji wa Mungu katika wote na yote. Imani inaona mambo yalivyo, si yanavyoonekana kwa nje tu. Imani inamuona Mungu na kusababisha sala, hasa ikijaa unyenyekevu, yaani ikikubali ukweli hata unapotuumiza kwa kututambulisha unyonge wetu unavyohitajika kumtegemea kabisa

Mungu Muumba na Mkombozi.

**Wampende, wamheshimu, wamuabudu, wamtumikie, wamsifu, wamshukuru na kumtukuza**  
Vitendo saba vinavyotarajiwa kadiri ya Mt. Fransisko, alivyojaribu kuvirodhesha katika jitihada zake za kutokeza vilivyomtokea mwenyewe, kama mlipuko wa ndani mwake uliosababishwa na uwezo wa Utatu.

**Mungu Mkuu aliye juu kabisa na wa milele** Ni baadhi ya sifa za Mungu zilizomvutia sana mzee wetu hata akazama katika kuzizingatia kwa mshangao mpya daima.

**Baba na Mwana na Roho Mtakatifu** Kwa ufunuo wa Mungu sisi Wakristo hatuishii katika sifa zake, bali tunakaribishwa kumjua katika nafsi zake tatu, ndio uzima wa milele, alivyatueleza Yesu.

**Wakamuabudu kwa moyo safi** Neno hilo linarudia katika Kanuni kama linavyorudiarudia katika maandishi ya Mt. Fransisko, usafi wa moyo tu umeahidiwa heri ya kumuona Mungu.

**Kwa kuwa hakuna budi kusali daima bila ya kukata tamaa** Mt. Fransisko ametukumbusha hayo maneno ya Lk. 18 1 juu ya haja ya kudumu katika sala, litokee lolote lile, tusikate tamaa wala tusiache sala, kwa sababu ni swala la uhai au kifo. Tufanye juu chini ili sala isikome, tujitahidi kufa na kupona kwa sababu hakuna budi, alivyatufundisha Yesu mwenyewe.

**Maana Baba anatafuta watu kama hao wamuabudu** Kwa mara nyingine Mt. Fransisko ametushonea maneno ya Yesu Yoh.4 23, ambayo yalimgusa zaidi. Kufikiria kwamba Baba ana hamu ya kuona watu wa namna hiyo kulimfanya ajitahidi sana kumtimizia hamu kwa kumuabudu katika Roho na ukweli.

**Kwa roho hiyohiyo waadhimishe masifu ya Kimungu** Liturujia ya Vipindi inakusudiwa kuchochaea roho hiyo ya sala na kutakasa siku nzima, usiku na mchana. Kama makleri wengine, Mt. Fransisko na wenzake waliadhimisha Sala ya Kanisa, wakati mabradha walipokuwa wakisali Baba Yetu kadhaa. Siku hizi Kanisa linahimiza watawa wote na hata Walei kushiriki Liturujia ya Vipindi.

Hakuna tena shida ya lugha wala ya elimu. Tukumbuke jinsi Mt. Fransisko alivyojali kazi hiyo hata akawaruhusu watawa wake wawe na breviary ambazo ziliikuwa za ghamara kubwa ingawa aliwabania sana mavazi. Naye mwenyewe alijitahidi kutimiza wajibu wake kadiri alivyoruhusiwa na maradhi. Maandishi yake pia yanashuhudia msimamo wake

**Wakiungana na Kanisa lote** Kwa mzee wetu kusali Liturujia ya Vipindi kulikuwa ishara ya Ukatoliki, hiyo ilikuwa sababu nyingine ya kusisitiza uaminifu kwa sala hiyo. Kwa jumla ni kwamba tunaposali Masifu tunaungana na sala rasmi ya Kanisa na kuonyesha tunavyokubali kuongozwa nalo hata katika uhusiano wetu na Mungu. Mt. Fransisko alipenda kusisitiza ushirika wetu na Kanisa la Roma kwa kuagiza Ndugu Wadogo wafuate mtindo wa Kanisa hilo, badala ya ule wa jimbo lolote au wa shirika. Ndani ya Kanisa, chini ya taratibu zake tunaungana na Yesu mwenyewe anayesali kwa njia ya viungo vyake.

**Wowote wale** Yaani Ndugu wa Kiume na wa Kike, bila ya ubaguzi.

**Ambao Bwana amewaita kwenye maisha ya sala hasa** Huo ni wito ndani ya wito wa msingi wa Kifransisko. Baadhi ya Ndugu wa Utawa Hasa wa Tatu wanaitwa kukazania sala hata kuacha utendaji wa nje. Toka mwanzo tunakuta watu wenyewe wito huo, k.mf. katika makao ya upwekeni. Baadaye wanawake wakaanzisha hata monasteri za TOR. Hata leo wito huu ni muhimu kwetu sote. Ndiyo sababu unazungumziwa katika kanuni. Ni heshima ya wenyewe wito huo, na pia ni utajiri wa Utawa mzima na changamoto kwetu sote tufanye kazi ya sala vizuri kuliko nyingine zote, kwa kuwa ndiyo kipaumbele.

**Waonyeshe kwa furaha mpya daima** Katika faraja na katika ujavu, katika mafanikio na katika majoribu. Furaha ya Kikristo na ya Kifransisko, tuliyofundishwa, ni ile inayokamilika katika msalaba, na inayotegemea imani.

**Kuwa wamewekwa wakfu kwa Mungu** Waliojiteteng na ulimwengu ili kuzama katika sala, hasa, na kwa namna ya pekee wanawake waliojifungia ndani, wanaonyesha vizuri kabisa walivyowekwa wakfu kwa Mungu tu. Katika maisha yao hakuna mwagine au kingine Basi wafurahie kiimani hali yao. Ndio ushuhuda wao wa kitume.

**Nao waadhimishe upendo wa Baba kwa ulimwengu** Ndicho tunachoadhimisha hasa, kama vile ndicho tunachotangaza kokote. Kwamba Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanae awe kipatanisho cha dhambi zetu. Liturujia ni adhimisho la fumbo hilo la Pasaka kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

**Yeye aliyetuumba, aliyetukomboa na atakayetuokoa kwa rehema yeke tu** Maneno hayo ya Mt. Fransisko yanasisitiza kwamba Mungu tu anaweza kufanya hayo. Mangamuzi yalimfanya aone kila mtu kuwa hafai kitu, kuwa sisi sote ni maskini na wanyonge, wenye kuoza na kunuka, tusio na shukrani na waovu. Kwamba Mungu anatupenda tulivyo, ndilo ajabu la maajabu linalostahili kuadhimishwa pasipo kuchoka, wala kuzoea, kwa furaha mpya daima.

**10.** Para hii inatutaka tumsifu Mungu kwa uumbaji wake, hasa kwa jinsi alivyotuumba sisi kwa sura na mfano wake.

**Ndugu wa Kiume na wa Kike wamsifu Bwana, mfalme wa mbingu na nchi** Mt. Fransisko alipenda kumuita Mungu hivyo, kufuatana na maneno ya Yesu mwenyewe. Yeye ni mfalme mkuu, ni muumba wa vyote, vya juu na vya chini, vya kiroho na vya kimwili. Tena ni Baba yetu. Mt. Fransisko alijaliwa kufurahia ukweli huu kwa namna ya pekee.

**Wakiungana na viumbe vyake vyote** Mzee wetu alialika wote wenye akili na utashi waungane na viumbe vyenzao visivyo na akili amba wanamsifu mfululizo Muumba wao kwa kufuata amri zake.

**Nao wamshukuru kwa kuwa kwa matakwa yake matakatifu na kwa njia ya Mwanae wa pekee pamoja na Roho Mtakatifu** Baada ya kumsifu Mungu kwa kazi yake ya kuumba viumbe vingine, tunapaswa kumshukuru kwa kutuumba sisi wenyewe. Tunashukuru kwa zawadi ya uhai aliyotujalia. Ndivyo Baba alivyotaka na alivyofanya kwa kushirikiana na Mwana na Roho Mtakatifu. Mt. Fransisko alikiri wazi kuwa uumbaji ni kazi ya Utatu Mtakatifu mzima. Nafsi tatu ni umoja hata katika utendaji wa nje ya Umungu.

**Ameumba vyote, vya kiroho na vya kimwili, nasi kwa sura na mfano wake** Mungu, kisha kuumba aina hizo mbili, ametuumba sisi tulio mchanganyiko wa roho na mwili, jambo la ajabu sana. Hivyo kati ya viumbe vinavyoonekana, sisi tu ni sura na mfano wa Mungu, tuna heshima ya pekee ya kumjua na kumpanda na kumtumikia kwa hiari, pamoja na kutawala dunia. Ndiyo sbabu tunapaswa zaidi kumshukuru kwa maneno na matendo.

**11.** Waandishi wa maisha ya Mt. Fransisko wanasisitiza kwa haki jinsi alivyozama katika Maandiko Matakatifu. Para hii inatuelekeza kumuiga, kwa kuwa wito wetu ni kujilinganisha na Injili, jambo ambalo haliwezekani tusipotafakari Neno la Mungu, ili lisomeke katika mwenendo wetu.

**Ndugu wa Kiume na wa Kike, wakijilinganisha na Injili** Ndio msingi wa maisha yetu, tulivyosikia tangu sura ya kwanza. Sio tu kushika amri, bali kujilinganisha kabisa.

**Wazingatie na kutunza akilini** Kama alivyofanya Bikira Maria maisha yake yote. Mt. Fransisko alimchukua kama kielelezao kwake na kwetu.

**Maneno ya Bwana wetu Yesu Kristo, aliye Neno wa Baba, na maneno ya Roho Mtakatifu yaliyo roho na uzima** Mt. Fransisko alipowaandikia Ndugu wa toba toleo la pili la himizo lake alitumia maneno hayo ili kusitisitiza kwamba hakuwatumia ujumbe huo, kama wa kwake, bali ni wa Mungu. Maisha yake yote yalitegemea Neno la Mungu, hivyo alihimiza kulipokea hata kwa njia ya maandishi yake. Si kupokea maneno fulanifulani tu, bali kwa njia hiyo kumpokea yule aliye Neno wa Baba na pia Roho Mtakatifu, kwa kuwa katika Neno la Mungu tunapata roho na uzima. Tukiwa na hakika hiyo, tutaungana na Wafransisko wote ambaa daima wamejali sana Neno katika maisha ya sala na ya kiroho.

**12.** Bila ya shaka muungano na Mungu unafanyika hasa katika ekaristi. Mt. Fransisko katika maandishi yake yote alisisitiza heshima ya pekee kwa fumbo hilo Kanuni ya kudumu tu haihitaji kutokana na haja ya kuiandika kifupi na kisheria kwa muundo. Para hii inatumia baadhi ya maandishi hayo Kanuni ya muda 20 5, Barua kwa Shirika lote 12 13, Barua kwa Makleri 1, Wasia 12 ili kutuhimiza sisi pia tudumishe mapokeo hayo bora, yaliyoathiri Kanisa lote, pamoja na yale ya kuyaheshimu majina matakatifu, hasa lile la Yesu.

**Washiriki sadaka ya Bwana wetu Yesu Kristo** Hiyo ni sheria ya Kanisa kwa waamini wote kila Jumapili na kwa watawa kila siku, ikiwezejana. Lakini hasa ni haja ya imani na upendo. Misa ndiyo sadaka ileile ya msalabani, nasi tunapewa nafasi ya kuishiriki wenyewe kila leo. Nani anaweza kupuuzia nafasi ya namna hiyo. Tunaalikwa kuishiriki kwa dhati, sio tu kuhudhuria kama kwamba hatuhusiki, wala sio tu kuitikia kwa sauti bila ya kuchomwa moyo.

**Na kupokea Mwili na Damu yake** Mt. Fransisko hakutumia kamwe jina ekaristi kuhusu sakramenti kuu. Alipenda zaidi kutumia maneno ya wazi aliyoatumia Bwana mwenyewe Mwili na Damu. Tunahimizwa

kuvipokea. Mzee wetu, kufuatana na Mtaguso Mkuu wa IV wa Laterano aliohudhuria, alisisitiza sana haja hiyo kea wokovu wetu, wakati ambapo waamini walikuwa wameridhika na tendo la kutazama Hosytia takatifu mara baada ya mageuzo, bila ya kuitikia mwaliiko ya Yesu wa kumpokea katika sakramenti.

**Kwa unyenyekevu na heshima sana** ndiyo misimamo aliyodai Mt. Fransisko. Inatokana na kutambua unyonge wetu na ukoo wa Yule tunayetaka kumpoke.

**Wakikumbuka Bwana alivyosema, Anayekula mwili wangu na kunywa damu yangu ana uzima wa milele.** Mt. Fransisko alidondo neno hilo la Yesu Yoh. 6 54 linaloonyesha wazi jinsi ekaristi ilivyo chakula cha uzima wa kweli, ule wa Kimungu unaodumu milele. Siri ya mafanikio yake katika utakatifu ametutobolea hapa. Heri ytu tukijua kufaidika kweli na sakramenti hiyo kuu ambayo ni Yesu mzima.

**Kadiri ya uwezo wao waonyeshe kila heshima na kila ibada kwa Mwili na Damu takatifu sana ya Bwana wetu Yesu Kristo** Kwa sababu uwezo tulio nao hautoshi kabisa kuheshimu na kuabudu ekaristi inavyostahili. Walau tujitahidi upeo. Alipoliandikia shirika lote himizo hilo, Mt. Fransisko alisema anatushi wote akitibusu miguu na kwa upendo wote aliokuwanaao. Wafuasi wake walipokea neno hilo hata wakaliambukiza Kanisa lote. Ibada kwa ekaristi ni mojawapo kati ya maendeleo muhimu zaidi ya maisha ya kiroho ya waamini wa Magharibi.

**Na kwa maandishi yenyenye majina matakatifu na maneno yake** Mzee wetu akikaribia kufa alipotuandikia wasia wake hakusahau kutuachia mfano wake wa kuyakusanya hayo ili kuyaweka mahali pa kufaa, pamoja na kutuachia ombi la kufuata mfano wake, tusije tukayakanyaga. Kwa kuwa sisi binadamu katika ujinga wetu tunashindwa au hatutaki kuelewa ukoo wa Mungu na wa mambo yote yanayomhusu. Ndiyo sababu tunayataja bure na kuyatupa pasipofaa. Tungekuwa na imani....

**Ambaye ndani mwake viumbe vilivyopo mbinguni na duniani vimepata amani na kupatanishwa na Mwenyezi Mungu** Mzee wetu akiendelea kutuhimiza tuishi kiekaristi alitumia maneno ya mtume Paulo kwa Wakolosai 1 20 kuhusu nafasi ya kwanza ya Kristo katika yote. Akifanya hivyo ametuachia moja kati ya mafundisho yake bora, kwa kuonyesha jinsi huyo Mwana wa Mungu aliyefanyika mtu anavyoendelea kuwemo katika ekaristi kama kipatanisho, cha viumbe vyote.

**13.** Baada ya kumzungumzia mpatanishi pekee kati ya Mungu na wanadamu, kanuni yetu inamalizia sura ya tatu kwa para hii juu ya toba. Kihistoria, sisi watu ni wakosefu, hivi hatuwezi kumuendea Mungu kama waliviotakiwa kufanya Adamu na Eva kabla ya dhambi asili. Sisi wanae, maisha yetu duniani ni ya toba. Kwa mara nyingine kanuni inachota kwa wingi maneno ya Mt. Fransisko kuhusu utekelezaji wa adili hilo.

**Halafu katika makosa yao yote, Ndugu wa Kiume na wa Kike** Ni wajibu wa kila mmoja wetu kutubu kwa kila kosa, sio baadhi tu.

**Wasichelewa** Mt. Fransisko alipotoa mawaidha hayo XXII,3 kwa wafuasi wake alisema ni mtumishi mwaminifu na mwenye busara yule asiyechelewa kutubu. Kumbe uzembe wetu unatuacha tumelala chini, bila ya kujali hasara ya kuzidi kutawaliwa na dhambi na shetani.

**Kujiadhibu** Adhabu ndiyo dawa ya dhambi. Tusipojiadhibu, tutapatwa na adhabu bila ya kutaka na pengine hata bila ya kufaidika nayo. Kumbe tukijiadhibu tunarekebisha tulichoharibu na tunaendelea safari yetu kwa baraka ya Mungu.

**Kwa ndani kwa njia ya majuto** Toba inaanza moyoni kwa kuzingatia kweli za imani kuhusu dhambi imemchukiza nani, imeharibu nini, n.k.

**Na kwa nje kwa njia ya ungamo** Ungamo kwa Ndugu tuliyemkosea na kwa wale tuliowakwaza, pia kwa padri anayewakilisha Kristo katika kitubio. Bila ya hayo, toba ni ya wasiwasi, kwa kuwa inakosa unyenyekevu wa kukiri kwamba tumekosa. Hivyo ni rahisi zaidi kurudia dhambi. Ungamo linaimarisha majuto na nia ya kujirekebisha, linakomaza unyenyekevu na kuvuta neema. Akiona umuhimu wa tendo hilo, Mt. Fransisko alitaka Ndugu akimkosa padri kwa sakramenti, amuungamie kosa mwenzake.

**Nao wazae matunda halisi ya toba** Mzee wetu alizingatia sana maneno hayo ya Injili Lk. 3 8, kwa kuwa alijali sana ukweli wa mambo yote. Tusiridhike na toba ya mawazo na maneno, bali tuhakikishe kwamba inazaa matendo ambayo kweli yanabadili utu wetu ulingane na Mungu, na matakwa yake

**Wanapaswa pia kufunga chakula** Hilo ni mojawapo kati ya matendo ya toba . Katika Biblia mfungo ni msingi pamoja na sala na sadaka. Faida zake ni kumnyenyekea Bwana, kuijandaa kusali na kuelewa Neno la

Mungu, kuomba msamaha, kukabili wajibu mgumu, kuijandaa kutoa na kupokea neema zinazohitajika kwa utume Fulani n.k.

Hasa maisha ya Kiinjili yanadai mfungo, kwa kuwa Yesu mwenyewe alifunga chakula, alifundisha namna ya kufunga kwa kumpendeza Mungu, pia alitabiri kuwa rafiki zake watafunga. Basi, Mt. Fransisko akawa anafunga karibu mfululizo na kuagiza Ndugu zake wafunge chakula, ingawa hakueleza kinaganaga masharti ya mfungo, kufuatana na mfano wa Yesu wote wawili walitegemea unyofu wa moyo na bidii ya wafuasi wao kuliko sheria. Pamoja na kupendelea uhuru wa Injili, Mt. Fransisko alifanya hivyo kwa kuwahurumia Ndugu zake amba wanasonicwa sana na maisha ya ufukara, kazi na utume kiasi kwamba miili yao haikosi nafasi ya kuteseka na kumtolea Mungu sadaka. Hata hivyo kwa Mt. Fransisko mfungo ni msingi wa maisha ya toba ya mfululizo, ambayo yaendelee hata mtu anaposhindwa kufunga kimwili.

Siku hizi, ambapo ulimwengu una starehe za kila aina, watawa pia wako hatarini kusahau umuhimu wa kutiisha mwili usije ukazuia roho isielekee utakatifu, bali ujaribu kulingana kabisa na roho kama ule wa Mt. Fransisko. Haja ya mwili kufanya toba pamoja na roho inaeleweka kwa urahisi tukizingatia udhaifu wa binadamu, upendo unaotusukuma kushiriki yote ya Bwana Yesu, na ushuhuda wa kitume.

**Lakini wajitahidi kuwa daima wanyofu na wanyenyeketu** Kanuni inakaza tena misimamo hiyo ya msingi ya Mt. Fransisko kwa kutumia maneno ya Himizo kwa Ndugu wa Toba toleo la pili, 45. Mfungo unaweza ukazaa kiburi na unafiki. Ndiyo sababu Yesu alituonya tufunge kweli kwa ajili ya Mungu, la sivyo hakuna faida yoyote Math. 6 16 18. Tukijisikia kufunga, kabla hatujaanza tuhakikishe kwamba nia hiyo inatokana na Roho Mtakatifu na kwamba wakubwa wetu wanatukubalia.

**Basi, wasitamani chochote kile isipokuwa Mwokozi wetu** Maneno hayo ni muhtasari wa yale ya Mt. Fransisko katika Kanuni ya Muda 23 9 ambayo kwa mara tatu **anatuangalisha** na chochote kile ambacho si Mungu pekee wa kweli. Yeye tu tumtamani, tumtake na kumfurahia, kwa kuwa yeye tu ni mwema. Kuachana na chochote kile kwa ajili ya Mungu ni namna nyingine ya kufunga. Kadiri tunavyojinyima malimwengu tunaweza kumtamani Mwokozi wetu, neno lake na mwili wake.

**Ambaye kwa damu yake mwenyewe alijitoa sadaka na kafara katika altare ya msalaba kwa ajili ya dhambi zetu** Kama kawaida, mzee wetu anatuelekeza kwa Yesu na ukweli wa maisha na mateso yake. Alitumia maneno hayo kuhusu ekaristi, chakula chetu cha kweli, katika Himizo toleo la pili, II 14 pamoja na yale yanayofuata. Sura hii inafikia kilele chake katika kutuvuta tumzingatie Kristo katika fumbo la Pasaka, ambalo tunamfikia Mungu kwa kuondolewa dhambi.

**Akituachia mfano kusudi tufuate nyayo zake** Maneno hayo ya mtume 1Pet. 2 21 yalimgusa sana Mt. Fransisko, hata akatamani kufuata kabis nyayo za Yesu. Kila mmoja wetu, anapozingatia Bwana alivyofanya, hasa katika ekaristi, anapawa kujitahidi afanye vivyo vivyo. Hapo, heri yake. Kama mzee wetu, ataweza kugeuka na kuwa Kristo yalingine.

### **SURA YA NNE MAISHA YA USEJA KWA AJILI YA UFALME WA MBINGUNI**

Katika sura ya tatu tumeona jinsi maisha ya sala yanavyotuelekeza kumfuata Yesu aliyejitoa sadaka. Sasa sura ya nne inatuonyesha namna ya pekee ya kujitahidi nyuma yake kama adaka hai ya kumpendeza Mungu, yaani kwa maisha ya useja kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Ndio msingi wa utawa wowote kama maisha yaliyowekwa wakfu kwa Mungu.

Kwa kuwa ndoa ni njia halali pekee ya kutekeleza jinsia kimwili, yejote anayejinyima ndoa anapaswa kushika usafi kamili, bila ya tofauti. Masharti ya utiifu na hasa ya ufukara yanaweza yakawa mbalimbali kadiri ya mashirika, lakini usafi katika useja ni uleule kwa wote. Hata hivyo Mt. Fransisko, akiwatuma wafuasi wake ulimwenguni wakatangaze toba kwa maneno na hasa kwa matendo, aliwadai sio tu wakwepe dhambi na hatari za kuzini, bali pia wajihadhari na chochote kile kinachoweza kikasababisha wengine wapatwe na shaka juu ya usafi wao, hasa upande wa mafungamano na jinsia ya pili. Hata leo, katika mazingira tofauti sana, Kanisa linadai kan.277 busara ili makleri na watawa wasihatarishe usafi wa moyo wao wala wasiwakwaze watu. Kwa ajili hiyo askofu wa jimbo anaweza kutoa mwongozo maalumu.

**14.** Para hii inaweka mbele yetu mtazamo wa Mt. Fransisko juu ya utu wetu, roho na mwili tukitambua tulivyoumbwa kwa njia ya Kristo na kwa ajili ya Kristo, tutaelewa namna ya kujiheshimu na manufaa ya kumfuata yeye hata katika jambo la pekee kama useja ulivyo.

**Ndugu wa Kiume na wa Kike wazingatie cheo kikubwa walichojaliwa na Bwana Mungu** Yaani

kwamba sisi ni tofauti sna na wanyama, ingawa mwili wetu unafanana na wa kwao, na maelekeo yake ni ya nguvu vilevile, hata kutufanya tusione ubora wa maumbile yetu. Tunahitaji kutulia na kuzingatia ajabu la utu wetu ulivyoumbwa na Mungu, kama umoja wa roho na mwili, tusije tukafuata tu kinachoonekana, na tamaa zake.

**Kwa kuwa aliwaumba na kuwaunda kwa sura ya Mwanae mpenzi katika mwili na kwa mfano wake katika roho** Maneno haya na yaliyotangulia yalitolewa na Mt. Fransisko kwa wafuasi wake kama Mawaiha 5 1, yaani kama ufanuzi wa Maandiko Matakatifu. Hivyo aliwashirikisha si usomi wake, bali undani wa sala yake, alivyotazama kazi za Mungu hasa katika mtu, kiumbe alichaoamua kushiriki maumbile na maisha yake kwa njia ya Mwanae mpenzi. Ndiyo sababu kwa Mt. Fransiskomaneno ya Mwa. 1 26 sura na mfano yanamhusu Yesu. Kadiri ya mababu, dhambi ya asili imetufanya tuendelee kuwa sura ya Mungu, lakini sio mfano wake tena, mpaka tukombolewe. Katika ufupi na uzito wa maneno ya Mt. Fransisko tunaelekezwa kuona kwamba ili tuwe mfano wake tunapaswa kuongozwa na Roho Mtakatifu kama Yesu. Hapo tutaheshimu mwili wetu pia kama sura yake.

**Wenyewe, walioumbwa kwa njia ya Kristo na ndani ya Kristo** ndio ukweli wa imani unaotufumbulia fumbo letu. Nje ya Kristo hatuwezi kujielewa. Ndiyo utimilifu wetu kama watu. Kwa msingi huo, na kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu kama yeche alivyofanya, tunaweza kushika hata useja ingawa mwili wetu unaelekea kwingine, hasa baada ya dhambi asili kutuvuruga kwa ndani.

**Wamejichagulia mtindo huu wa maisha** Yaani kwa hiari kabisa na kwa moyo mkuu wameamua kuishi kwa mtindo usio wa kawaida duniani, yaani bila ya ndoa, na ya yote yanayohusiana nayo.

**Ambao msingi wake ni maneno na mifano ya Mkombozi wetu** Yesu ametukomboa sio kiroho tu, bali kimwili pia, yaani anatuwezesha kushinda zaidi na zaidi maelekeo mabaya tuliyorithi, hata kuiga mifano yake mwenyewe. Yeye hakuoa, bali aliunda familia nyngine isiyotegemea ubinadamu ila imani, wale wote wanaotimiza mapenzi ya Baba kama yeye ndiyo familia ya Mungu. Ndiye kielelezo cha useja mtakatifu, nayefanya mtindo huo wa maisha kuwa bora kuliko yoyote, kwa kuwa ni namna aliyoshi Mungu duniani. Kwanza mtume Paulo 1Kor.7, halafu ualimu wa Kanisa hasa mtaguso wa Trento wamefundisha rasmi kuwa hali hiyo ni bora kuliko ndoa. Kumbe siku hizi wengi hawajui dogma hiyo, wala hawatambui ukweli huo sababu ni kwamba wanashau vurugu za jinsia zilizofuata dhambi asili, au wanakusudia kuwahimiza watu wa ndoa walenge utakatifu wa wito wao, au wanatazama maisha kibinadamu mno, n.k. Lakini Mtaguso wa II wa Vatikano umerudia kuonyesha useja kuwa ni njia ya kufaa zaidi katika kulenga upendo kamili. Ndoa ya Kikristo ni alama ya upendo kati ya Kristo na Kanisa, kumbe useja ndio utekelezaji wenyewe wa upendo huo. Katika ndoa mtu anapaswa kumpenda Mungu kwa kuititia viumbwe mwenzi na watoto, kumbe katika useja mtu anapaswa kumpenda Mungu tu moja kwa moja. Pamoja na hayo kujinyima ndoa au tendo lake kunachangia ustawi wa sala na nafasi ya kutoa huduma 1Kor.7 5, 1Tim.5 5,10 na kunamtolea Mungu mwili pia kama sadaka hai kwa namna inayozidi ile ya wanaowajibika kutimiza amri ya 6 na ya 9 1Thes. 4 3 8.

**15.** Para hii inaonyesha jinsi useja unavyosaidia utumishi wa Bwana na unavyotakiwa kujitokeza katika matendo yaliyojaa upendo. Kama vile ufukara unatuondolea mahangaiko tutulie katika kazi ya utakatifu.

**Kwa kuwa wamejifunga kushika useja kwa ajili ya ufalme wa mbinguni** Ndiyo lengo alilolitaja Yesu Math. 19 12. Maana yake ni kwa ajili ya kuufikia ufalme huo na pia kuueneza kwa urahisi zaidi. Kwa lengo hilo wamejifunga kwa hiari kushika useja.

**Wanatafuta yaliyo ya Bwana** Ya kwake peke yake, bila ya mgawanyiko wa nia na moyo.

**Na kutokuwa na kazi nyngine isipokuwa kutimiza matakwa ya Bwana na kumpendeza yeye** Maneno hayo ya Mt. Fransisko Kanuni ya Muda 22 9 yanatuletea mtazamo wake mnyofu. Kwa kuacha ulimwengu yaani kutawa maisha yanakuwa sahili, ni kumtii na kumpendeza Bwana tu.

**Basi, wafanye yote hivi kwamba katika matendo yao ungae upendo kwa Mungu na kwa watu wote** Hivyo itaonekana maana ya useja kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Upendo utathibitisha ubora wa useja mtakatifu. Useja unategemea upendo na kulenga upendo kamili. Ni muhimu kusisitiza uhusiano huo, hasa siku hizi.

Karne ya XX imeleta mengi tena makubwa yanayoweza kutumika vizuri au vibaya. K.mf. saikolojia elimunafsia imetusaidia kuelewa maelekeo yetu kuhusu jinsia na kuyakabili, ingawa wengine wameifanya iwe silaha ya kutetea uzinifu na kupinga uwezekano wa usafi wa moyo hasa katika useja. Kanisa linatuelekeza kufaidika na saikolojia kwa maisha yetu ya kiroho, ya kijumuia na ya kitume. Zamani umuhimu wa mapendo ya kibinadamu haukueleweka, hivyo wenye wito wa kitawa waliweza wakalelewa kwa vitishovitisho wasivunge

useja. Siku hizi unasisitizwa ukuzaji wa upendo halisi kama njia bora ya kutimiza jinsia na mapendo hayo. Huo upendo uwepo katika mafungamano, pasipo kupuuzia udugu na urafiki, yaani usiwe wa Kimungu tu, wala baridi mno. Mradi tu mtu awe macho atambue mapema urafiki unapoanza kuwa wa pekee na kuchochea tamaa za mwili, jambo linalokukubalika katika ndoa peke yake, Hivyo aliyemuahidia Mungu kujinyima ndoa ayazime maelekeo hayo kabla hayajasababisha kishawishi.

Mtaguso wa II wa Vatikano ulifundisha kwa kuchota ya kale na mapya. Upande wa useja umetukumbusha mangamuzi ya karne nyingi, ya kwamba watakatifu waseja walikomaa hata kiutu, kama wanaume na wanawake. Imekuwaje. Ni kwamba mtu si mwili tu na silica zake, bali kwa akili na utashi alivyojaliwa anapaswa kuongoza maelekeo yake na mapenzi. Jinsia inaweza kukamilisha utu ikiwatumika katika upendo halisi, la shivyo inamrudisha nyuma binadamu katika kutamani na kujipendea tu, Upendo huo unaweza kumkamilisha mtu bila ya tendo la ndoa, mradi asione kulikosa ni hasara, bali ni nafasi ya kumuelekea Mungu na watu wowote kwa namna nyingine, tena bora.

Basi, baada ya kupokea mchango wa elimunafsia ya kisasa, tupokee tena ujumbe wa watakatifu waliotutangulia, ambao walisisitiza juhudzi za mtu katika kushinda tamaa. Mt. Fransisko alihimiza kuzificha na kulinda kwa uangalifu mkubwa hisi zote zisiwe milango ya mauti ya roho. Alikataza mafungamano yale ambayo yanadroofisha watu imara na kuangusha walio dhaifu, akikumbusha Neno la Mungu kuhusu ugumu wa kushirikiana na jinsia ya pili bila ya kuvutiwa visivyo na maumbile yake. Sanasana alikubali wanawake wapewe kitubio na mashauri mafupi ya kiroho. Upande wake aliyakatalia macho yake yasitazame sura zao, isipokuwa za wawili, akiogopa kumbukumbu na ubunifu vitazifanyia kazi na kuchochea tena mwili.

Mfano wake utusaidie kuchambua yale yanayotaka kuingia ndani mwetu, ili tukwepe iwezekanavyo yale yasiyofaa, hasa tukizingatia kwamba siku hizi miiko mingi imekwisha, na vyombo vyaya upashanaji habari vinaeneza kwa urahisi mkubwa chochote kile. Hivyo inahitajika nidhamu kubwa ya binafsi na busara nyingi, hasa katika nafasi zile ambazo zinaonekana kueleweka, kumbe kwa chini zinaelekeza dhambini. Nidhamu inamtaka mtawa awe mtaratibu katika maneno na matendo, hata wengine waelewe mara msimamo wake na kumuacha salama. Kanzu ikitumika vizuri inachangia sana usalama huo.

Usafi wa moyo unafungamana na maadili mengine na kuwa na masharti mbalimbali ambayo tutayataja baadhi yake. Kwanza kukwepa mitindo ya ulimwengu katika matendo, maneno, masomo, urafiki n.k. Tuukabili ulimwengu kwa utulivu na bila ya hofu, lakini tusisahau kuwa usafi wa moyo unampa ushindi anayekimbia vishawishi tofauti na maadili mengine, waliopuuzia ukweli huo waliokota dhambi tu, hata jumuia nyingi zikasambaratika. Mungu anaweza akamsaidia mtume wake anayekabili hatari ili kuokoa watu, akisali kwa unyenyekevu, lakini halazimiki kumsaidia mtu asiyeha na busara akijidai kwa kiburi kuwa haogopi hatari.

Sharti lingine ni matendo ya toba, yaani kujinyima vitu halali ili kuwa tayari kujinyima dhambi, kwa namna ya pekee upande wa chakula, kwa sababu ulafi. Ulevi na uzinifu vilevile ni tamaa za mwili zinazotakiwa kushindwa na adili la kiasi. Anayeshinda ulafi anashinda kwa urahisi fulani uzinifu pia. Mtaguso wa II wa Vatikano umesitisiza tena umuhimu wa kutawala hisi na wa masharti mengine ya mapokeo ya Kanisa. Sawa na raidha na michezo, usafi unahitaji mazoezi ili kufanikiwa.

Sharti lingine ni utaratibu wa maisha ambapo sala na kazi, utume na pumziko vina nafasi maalumu ili kutumia muda wote kwa wokovu wa watu na utukufu wa Mungu. Pasipo mpangilio wa wajibu, ndugu akipoteza muda hasa kwa mazungumzo ya bure, akiahirisha daima nafasi za kukutana na Bwana, asipokusanya mawazo yake ili asali na kufanya kazi vizuri, si ajabu akipatwa na vishawishi. Jumuiani heshima na uelewano ni muhimu kwa usafi wa moyo. Lakini kujenga upendo si kuondoa nidhamu utawani ili kuchekachecha mfululizo badala ya kuwajibika, bali ni kushirikiana kwa furaha katika kulenga utakatifu wa wito wetu. Walatini walifundisha Dumisha utaratibu, nao utaratibu utakudumisha wewe. Bila shaka, mapumziko na maburudiko yanahitajika pia, ili mtu asijikaze kuliko uwezo wake wa kustahimili, kwa kuwa kuzidisha kazi na kujichosha mno kunasababisha hatari vilevile. Basi, ratiba ya jumuia inatupatia tayari mchanganuo mzuri kutokana na mangamuzi ya karne nyingi, tukiifuata vizuri itatusaidia sana kulinda usafi wa moyo na kungarisha upendo kwa Mungu na kwa jirani katika matendo yetu yote.

**16.** Para hii haina dondo maalumu la Mt. Fransisko, ila inafuata wazo la Himizo kwa Ndugu wa Toba, kwamba upendo wa mwanafunzi na Bwana unafanana na ule wa wanaarusi. Wazo hilo linatokana na Biblia, maandishi ya mababu na ya waalimu wa kiroho, nalo linatuvuta sana kutamani neema ya muungano wa dhati na mpenzi wetu Yesu Kristo.

**Wakumbuke ya kuwa wameitwa, kwa zawadi bora ya neema** Wito wa kitawa ni neema yenye thamani isiyopimika, ulivyosema Mtaguso ndiyo sababu ni rahisi kusahau ubora wake na kuzingatia tu ugumu wa kuitikia vizuri. Kumbe kukumbuka hilo kunatia shime katika majaribu ili kudumu kiaminifu.

**Waonyeshe katika maisha yao lile fumbo la ajabu la Kanisa, ambalo limeunganika na Kristo, Bwanaarusi wa Kimungu** Fumbo hilo ni kubwa Ef. 5 23 26. Ndoa ni mfano wa mapendano hayo, lakini useja unadhihirisha ukweli wake. Hasa mwanamke mtawa anaonyesha jinsi upendo wa Kristo unavyowashika baadhi ya wafiasi wake hata wasikubali uhusuano wa pekee na mtu mwngine, yaani mapenzi kwa mwenzi wa ndoa. Kwa ajili ya ufalme wa Mungu, ambako ndoa pekee ni ile ya Mwanakondoo na Kanisa, mtawa anatunza ubikira au anajifanya towashi, yaani anaacha kuzitumia nguvu za maumbile yake yanayomuelekeza kupendana na mwngine kiroho na kimwili na kuzaliana naye. Kwa akujinyima mema hayo anajitoa kwa Bwana tu ili kupendana naye moja kwa moja, kama linavyotakiwa kufanya Kanisa. Lakini si waamini wote wanajaliwa kuelewa na kutekeleza hilo. Wanaoweza ni kwa sababu Roho Mtakatifu anawavuta kwa Yesu hata wawe ishara ya kinabii ya ule ule upendo mkuu usio na mwisho.

**17.** Katika kuzungumzia useja mtakatifu hatuwezi kumsahau Maria, anayetajwa kwa heshima kwa kumuita Bikira. Ndiye hasa kielelezo cha Kanisa kama Bibiarusi wa Kristo. Para hii ni nafasi bora kwa kumweka mbale yetu atuonyeshe njia.

**Wakikazie macho hasa kielelezo cha Bikira Maria mwenye heri** Siyo tu upande wa ubikira wa mwili, bali zaidi upande wa ubikira wa imani na wa unyenyekevu wake. Ni mfano wa kuzingatiwa mfululizo kwa kuvutiwa macho ya moyo na uzuri wake.

**Mama wa Mungu na Bwana wetu Yesu Kristo** Uzazi huo wa ajabu ndio thibitisho kuu la ubora wa ubikira. Unapoonekana kufanana na utasa, kumbe unazaa Kimungu.

**Wafanye hivyo kadiri alivyaoagiza mwenye heri Fransisko** Mzee wetu ametajwa wazi kama mmojawapo kati ya wale waliohimiza zaidi kuzingatia kielelezo cha Maria. Yeye alimuona hasa kama mwanamke wa imani aliyetafakari na kutekeleza mfululizo Neno la Mungu, na yale yote yanayomhusu \yesu.

**Ambaye alimheshimu sana Maria Mtakatifu, bibi na malkia** Mpaka leo inatunzwa aina ya litania aliyoitunga Mt. Fransisko kwa ajili hiyo ikianzia na kumuita hivyo. Lakini hiyo ni mojawapo tu kati ya sifa nydingi alizomtolea.

**Aliyefanyika Bikira Kanisa** Yaani Maria amefanyika kielelezo cha Kanisa lote, ulivyosisitiza Mtaguso wa II wa Vatikano. Mt. Fransisko aliwahi kutumia maneno hayo katika litania hiyo ya salamu kwa mwenye heri Bikira Maria ambayo inafuatana na nydinge ya kusalimia maadili yote. Ni kama kudokeza kwamba Maria ni kielelezo cha maadili yote.

**Tena wakumbuke kuwa Bikira Maria asiye na doa** Sifa hiyo ya Kukingwa Dhambi Asili ilitetewa na Wafransisko dhidi ya wapinzani. Hivyo si ajabu kwamba kwa sifa hiyo Maria anaheshimiwa kama msimamizi wa utawa mzima wa Kifransisko. Ndiyo sababu anatajwa hivyo katika kanuni.

**Alijiita Mtumishi wa Bwana** Kwanza akimjibu malaika Gabriel, halafu akimshangilia Mungu mbele ya Elizabet. Katika maneno hayo mawili Fiat na Magnificat imefichika siri ya Maria na ya utakatifu wake, unyenyekevu na utiifu. Juu ya msingi huo maisha yote yanaweza kuwa wimbo wa kumtukuza Mwenyezi Mungu anayetutende makuu. Wimbo wake umetokeza vizuri yaliyomo miyoni mwa maskini wa Mungu wanaomtegemea yeeye tu.

**Nao wafuate mfano wake** Sio tu katika kujiita hivyo, bali katika kuwa kweli na kutenda daima kama watumishi wa Bwana.

### **SURA YA TANO NAMNA YA KUTUMIKIA NA KUFANYA KAZI**

Kabla ya Mt. Fransisko, mapokeo ya kitawa yalisisitiza sana kazi pamoja na sala. Akirithi sisitizo hilo, aliliingiza katika maisha ya kitume kati ya watu, na katika maisha ya udogo na ufukara, yaani katika jumla ya karama yake.

Hakuweza kusahau kuwa Yesu alitumwa na Baba halafu akawatuma wanafunzi wake kwenda ulimwenguni ndivyo Kanuni ya Ndugu Wadogo inavyosema kwa kuumaanisha utume. Kwa sababu hiyo, akisukumwa na Roho Mtakatifu, alijaambia wafiasi wake, twende ulimwenguni ili kuwahimiza wote, kwa mifano kuliko kwa maneno, watubu dhambi zao. Karibu sura zote za Kanuni hiyo zinamchora Mfransisko kati ya watu, akiwapa hasa ushuhuda wa udogo, ufukara na udugu, pamoja na kwamba anaweza akawatangazia pia neon la Mungu. Lakini kwa mzee wetu ushuhuda wa maisha ni muhimu kuliko kuhubiri, hivi kwamba hakuweza

kukubali ushuhuda uhatarishwe ili kuzidisha mahubiri. Kwake si ndugu wote wanaweza kuhubiri, lakini ndugu wote wahubiri kwa matendo. Watu wanaguswa na mifano kuliko na maneno, hasa siku hizi ambapo maneno yamezidi, tena mengi si ya kweli. Ndiyo sababu Mtaguso umewahimiza watawa wa leo wazingatie ufukara kama ishara inayoheshimiwa na wengi, kwa kuwa inaonyesha hatujitafutii faida katika dini. Mfransisko hana budi kuhakikisha anatoa ushuhuda wa maisha matakatifu kuliko kuridhika na maneno mengi au kazi nyingi. Kumbe Mt. Fransisko alitabiri kwa uchungu kwamba wengi, kwa kisingizio cha kuwafundisha wengine, wataacha wito wao, yaani unyoofu safi mtakatifu, sala takatifu na bibi yetu ufukara.

Yeye aliona kazi kama njia ya kuwapa watu mfano mzuri katika wasia alitaja lengo hilo kable ya lile la mapokee la kukwepa uvivu ulio adui wa roho na hivyo kuwahubiria toba kwa matendo. Hasa kwa sababu kazi alizokisudia ni zile zinazofanyika kwa udogo chini ya wengine na kwa ufukara bila ya kumiliki kitu, isipokuwa vifaa vya kazi, tena bila ya kudai malipo. Akizingatia mfano wa Yesu katika sehemu kubwa kabisa ya maisha yake, alitaka ufanya kazi za mikono mpaka mwisho wa maisha yake, kadiri ya uwezo wake kama mgonjwa mwenye madonda ya Yesu. Katika wasia alitamka nia yake hiyo akaongeza, Vilevile nataka kabisa ndugu wengine wote wafanya kazi yoyote, lakini isiyoleta kikwazo, wasiojua kazi, basi wajifunze.

Utawa wa Tatu unashiriki mtazamo huo, lakini unaunganisha na jambo lingine muhimu la mapokeo yake, yaani huduma au matendo ya huruma kwa wanaohitaji msaada. Hayo matendo ni sehemu muhimu ya maisha ya toba. Uongofu wetu kwa Mungu unapimwa na upendo wetu kwa jirani 1Yoh. 4 20, kwa kuwa Mungu ni upendo, hasa kwa maskini. Kama vile Mt. Fransisko alivyotaja katika wasia huruma aliowafanyia wakoma kuwa ndio tukio kuu la uongofu wake, Ndugu wa Toba waliomfuata walijitao mfululizo katika kusaidia fukara na wagonjwa na kuleta amani kati ya watu. Ndiyo sababu kichwa cha sura hii kinataja, kama kile cha sura ya 7 ya Kanuni ya Muda, kutumikia pamoja na Kufanya kazi.

Tofauti na wamonaki, Wafransisko kwa kawaida wanaishi kwa kushirikiana na watu, ingawa kwa namna inayopinga ile wanayoishi hao. Hasa chaguo la kupendelea watu wadogo, kusimama upande wao katika ulimwengu wa matabaka, hata kuchanganyikana nao katika kuwahudumia na kufanya kazi duni, linabainisha karama ya udogo na kudhihirisha toba inadai nini ili kuingia katika ufalme wa mbinguni. Wakati Injili inatoa mashauri kadhaa, udogo Math. 19 14 na matendo ya huruma Math. 25 31 46 ni masharti kabisa, ambayo tunapaswa kuyatimiza na kuyatangaza kwa wote.

**18.** Karibu maneno yote ya para hii yanatokana na Kanuni ya Kudumu 5, 1 2 na yanalenga kutukumbusha kwamba kazi si kwa ajili ya uchumi kwanza, wanavyodhani wengi. Bali ni kwa ajili ya ustawishaji wa utu mzima, hasa roho katika uhusiano wake na Mungu. Kwa kufanya kazi, kadiri ya mpango wa Mungu, sio tu kwamba mtu anapata vitu vingi zaidi na zaidi, bali anashirikiana na Muumba katika kuboresha ulimwengu na kwa njia hiyo anajikomaza pamoja na wenzake ili kujiandaa kwa uzima wa milele. Baada ya dhambi asili, ushirikiano huo unafanyika kwa uchovu, lakini adhabu hiyo inaweza kupokewa na kutolewa kama malipizi ya dahmbi zetu na za wenzetu, Kwa ufupi, kiutu kazi ni ya lazima kwa kukomaa, na kidini ya lazima kwa kufanya toba.

**Kama fukara** Maneno hayo mawili yalitumika na Mtaguso katika kueleza kwamba ufukara wa watawa wowote unashiriki ule wa watu wanaolazimika kufanya kazi ili kujipatia riziki kwa ajili yao na ya familia zao. Ikiwa hiyo ni kweli kwa watawa wote, zaidi tena kwetu watawa wa watu wadogo.

Kazi, maana yake ni utendaji wowote unaochangia ustawi wa binadamu, mmojammoja na katika jamii, upande wa mwili, wa akili na wa roho. Anayefanya kazi kwa mikono akilima au kujenga, mwalimu anayefundisha, msanii anayetumia vipawa vyake ili kutajirisha akili au roho ya wenzake, padri anayeshughulikia wokovu wa milele, na sista anayejitoa mhanga katika sala na toba, hao wote si wanyonyaji wasiostahili kula, kama walivyo wanaopoteza muda na vipaji walivyojaliwa na Mungu. Kuingia utawani si njia halali ya kupata riziki kwa hakika bila ya kutoka jasho. Ufukara wa Kiinjili unadai kazi, ilivyowekwa wazi hata katika sheria za Kanisa.

**Ndugu wa kiume na wa kike ambao Wana amewajalia neema ya kutumikia au kufanya kazi** Kama tulivyoeleza, kazi ni muhimu kabisa kimaisha, hasa kidini Si laana, bali ni neema ya Mungu. Kiasi kwamba tunapaswa kuwasikitikia wale wanaoikosa au wasioiweza. Hasa elekeo la kimaumbile katika kutumikia watu ni muhimu kulistawisha.

**Basi watumikie na kufanya kazi kwa uaminifu** Kama ilivyo kwa neema nyingine, hiyo pia inamdaidu aipokee kwa uaminifu. Maana ya neon hilo ni walau mbili Kwanza, kufanya sawa na anavyotaka aliyeagiza kazi yaani kwa mtawa ni Mungu akiwakilishwa na mhudumu wa shirika, pili, kufanya kwa bidii, yaani kwa kutumia nafsi nzima akili, utshi, vipawa na nguvu, hivi kwamba kazi yoyote ifanywe vizuri iwezekanavyo, sio ili mradi, bali kwa uangalifu kwa kuwa inafanywa kwa ajili ya Mungu.

**Huku wakimuabudu** Mangamuzi ni kwamba kazi ina uwezo wa kumshika mtu kupita kiasi, hata ikamsahaulisha Mungu anayemfanyia kazi. Sababu mojawepo ni kwamba inafanyika katika mambo yanayoonekana, kumbe Mungu haonekani. Lakini shida kubwa zaidi ni kwamba inaweza ikafanyika ili mtu ajiridhishe au kujikuza. Dhidi ya hatari hiyo, kanuni inadai moyo wa ibada, yaani wakati wa kazi Mfransisko azidi kumuabudu Mungu na kumkumbuka kwa upendo, akizua mawazo yake yasitawanyike katika kazi. Neno la mapokeo ya kitawa linaludi kutuonya, Usali na kufanya kazi. Muungano na Mungu hauhatarishwi na kazi yenyewe, ispokwu tukiifanya kwa lengo lililotofauti na Mungu, au harakaharaka bila ya utaratibu wala utulivu.

**Ili wakwepe uvivu ulio adui wa roho** Mt. Fransisko hakudharau mapokeo ya wamonaki, ingawa alijisikia wito tofauti. Ndiyo sababu aliweza kuingiza katika kanuni na wasia onyo hilo kuhusu tabia ya kupoteza muda. Uvivu ni kilema kikuu kimojawapo, ambacho kinazaa dhambi nyingi, tena ni vigumu kuachwa, hivyo ni adui wa roho. Mzee wetu alingamua ndugu ambaao ni mzigo kwa wenzao, wanapoteza muda na kufanya dhambi kwa mawazo na, hata akawatungia jina la ndugu nzi wanaofanya kazi kwa neon kuliko kwa mikono, wanakula jasho la wengine na sadaka za fukara, wanajua tu ratiba ya mezani na huwa wamechoka kabla hawajaanza kazi.

**Lakini wasizimishe ile roho ya ibada na sala takatifu, ambayo ni lazima iwe lengo la malimwengu yote** Maneno hayo yanaweka sala katika nafasi inayostahili, yaani ile ya kwanza, kwa kuwa Mungu ni wa kwanza daima. Katika utekelezaji, ni jambo gumu kuifanya kazi iwe ngazi, sio kizuo kwa kumfikia Mungu. Linategemea sana uaminifu katika kushika katiba na ratiba, pia uangalifu wa wahudumu ambaao wasiwaitwishe baadhi ya watawa kazi nyingi mno wala kuwaruhusu wazame katika shughuli, bali wawe na uwiano mzuri katika majukumu mbalimbali ya maisha yao.

Shida ni kwamba utendaji unavuta kuliko sala, watu wanavuta namna inayosikika kuliko ile ya Mungu, utendaji wa kibinadamu unaotegemea vyombo na vifaa unaeleweka kwa urahisi kuliko imani inayotegemea neema ya Mungu tu. Hata katika utume Mfransisko anapaswa kufanya mfululizo utambuzi wa matakwa ya Mungu, kwa kuwa utume si kazi yabinadamu bali ya Kimungu, watu hawaokolewei na maneno yetu matupu bali na neema ya Mungu inayotolewa kwa sala na stahili za watakatifu, zenye kutegemea zile za Yesu. Matunda mema, mengi na ya kudumu yanapatikana katika mti mwema, yaani mtu aliyeunganika kabisa na Yesu kama tawi na shina lake katika kufanya atakalo Baba tu. Jamaa kwa pamoja ichague na kutekeleza kidugu kazi zile zinazolingana zaidi na udogo na ufukara wetu, bila ya kupunguza juhudji katika sala na toba. Hapo matunda ya kiroho na ya kitume yatakuwa mengi ajabu, historia inavyoshuhudia.

**19.** Para hii inaendelea kufuata sura ya tano ya Kanuni ya Ndugu Wadogo kuhusu kazi. Baada ya kueleza namna ya kufanya kazi ili kuungana na Mungu, tunasikia tufanye nini kuhusu malipo yake. Uchumi si lengo, bali ni matokeo ya kazi. Basi, tuutazame vipi kama Wafransisko. Mzee wetu aliweka masharti ambayo yazuie utawa usitajirike, akiona kwamba monasteri nyingi kwa njia ya kazi zilipata mali nyingi. Kumbe yeye alitaka wafuasi wake washughulike bila ya kuhangaikia ya kesho, wakimuachia Mungu awalishe na kuwavika kama vile ndege na maua.

**Basi, kama malipo ya kazi** Mazingira ya maneno hayo ni Mfransisko kufanya kazi kwa ajili ya tajiri, hasa kazi za kibarua.

**Wapokee mahitaji ya mwili** Kanuni yetu haikariri maneno makali ya Mt. Fransisko kuhusu mwiko wa hela, lakini inatudai tupokee tunayohitaji tu, si zaidi. Udhafu wa mwili unahitaji chakula, mavazi, matibabu n.k. walau kwa kiasi fulani ambacho, kadiri ya mtume Paulo, turidhike nacho. Lakini kiasi kipi. Jibu liwe nyofu mbele ya Mungu, la sivyo ufukara utakwisha haraka, na matokeo yake yatakuwa kulegea kiroho katika yote, kwa kuwa tamaa za mwili na za macho zinapingana na tamaa za roho. Binadamu anaelekea daima kulimbikiza vitu na kujipatia maisha ya kupendeza zaidi, hata mtawa na shirika zima wanaelekea kudhani ni vya lazima vitu vingi zaidi na zaidi.

Basi, kuhusukutambua vipi ni vy lazima siku hizi, Mtaguso wa II wa Vatikano ulikariri maneno ya mwenye heri Yohane XXIII, Wajibu wa kila mtu, tena wajibu unaombana Mkristo hasa, ni kupima vissivyo vya lazima kwake kwa kuzingatia shida za wenzake Gaudium et Spes, 69. Ndicho kipimo alichotumia Mt. Fransisko, asikubali kuona mtu fukara kuliko mwenyewe. Hivyo ufukara haubaki katika nadharia, mbali na hali halisi ya maisha ambayo Yesu anayaishi leo katika wenye njaa na kiu, walio uchi n.k. Akiwa ndani mwao, mwenyeweanatuhimiza mfululizo tumshirikishe tulivyonavyo vyote na hivyo tujikomboe kutoka tamaa yoyote, isipokuwa ile takatifu ya kufaulu kumpenda jirani kama tunavyojipenda.

**Kwa ajili yao wenyewe na ya ndugu zao wa kiume na wa kike** Kama wanajumuia, tunapaswa

daima kuwafikiria wenzetu, hasa wasioweza kujipatia mahitaji yao kwa sababu ni wagonjwa, wakongwe au wanawajibika katika mambo yasiyoleta faida kiuchumi sala, utume n.k.. Tunaweza kuwapokelea mahitaji yao pia.

**Tena kwa unyenyekevu, jinsi inavyowapasa watumishi wa Mungu na wafuasi wa ufukara mtakatifu sana** Ndiyo msimamo wa Mt. Fransisko kuhusu malipo ya kazi juu ya msingi wa unyenyekevu na ufukara. Ni kwamba kazi ni neema ambayo mtu akiipokea hamtumikii mtu mwininge tu, bali Mungu hasa. Tukiwa watumishi wa Mungu tutarajie kulipwa naye, tusimda tajiri wala kulalamikia malipo anayotupa, bali tupokee kwa shukrani chochote kile na hivyo tuonyeshe wazi kuwa tunafanya yote kwa ajili ya Mungu, siyo kwa kupata thawabu ya watu. Wafanyakazi wa kawaida wana haki ya kulipwa sawasawa na kujipatia maendeleo, kumbe Mfransisko anatetea haki za wenzake, lakini si za kwake mwenyewe, na kwa ushuhuda huo unawafikirisha zaidi wanyonyaji.

Kwa uhuru huohuo wa wana wa Mungu tunatakiwa kuchagua kazi zile zinazolingana zaidi na wito wetu, sio zile zinazoleta faida kubwa zaidi kiuchumi. Lengo la kujitegemea lisituzuie kufanya kazi isiyo na malipo kama vile kufundisha dini au kuhudumia maskini. Tutafute kwanza utawala wa Mungu na uadilifu wake, na mengine tutapewa kwa ziada.

**Halafu yale yote yanayozidi wajitahidi kuwagawia maskini** Kwa kuwa ndiyo haki yao, alivyosisitiza Mt. Fransisko. Kwa kutumia Lk. 11 41, ye ye alidai tuendelee kuwasaidia masikini hata baada ya kuwagawia mali zetu zote. Kwa kuonja shida zao, tuzidi kuwaonea huruma na kuwasaidia kila tunapoweza. Hiyo itatusaidia kuzuia pia utajiri jumuiani.Tubane matumizi yetu ili kuwasaidia zaidi. Ndiyo njia ya kufikia upendo kamili, lengo la maisha yetu. Mtaguso unadai watawa wote wapende maskini katika tumbo la Kristo, yaani kutoka ndani na kutokana na upendo wetu unaotunganisha naye.

**Tena hawatakiwi kamwe kutamani wawe juu ya wengine** Maneno hayo na yafuatayo yamo katika toleo la pili la Himizo kwa ndugu wa Toba 47. Yanalingana na yale ya Kanuni ya Muda 7 1 2. Ni kwamba udogo unatuelekeza kinyume. Tusipende kutawala wengine hata kazini, ingawa tunaweza tukatafutwa ili tusimamie watu. Zamani za Mt. Fransisko, makardinali na wengineo walianza kuomba Ndugu Wadogo waendeshe nyumba na watumishi wao, lakini ye ye alikataza. Zaidi tena tusiwe na maboi jikoni, shambani, mlangoni n.k., ingawa visingizio vinaweza vikawa vingi k.mf. kile cha kufanya utume mwangi zaidi, ambacho hakizingatii kuwa ushuhuda wa udogo ni muhimu kwetu kuliko mahubiri, ila tunaweza tukamuita fundi kwa kazi fulani inayotushinda.

**Bali wanapaswa kuwa watumishi na kukaa chini ya kila mtu kwa ajili ya Mungu** Ndiyo nafasi yetu tulioitiwa, ile ya mwisho. Mt. Fransisko alipenda sana maneno hayo ya 1Pet, 2 13 kujishusha kwa ajili ya Mungu kama alivyofanya Mwanae aliyejitoa kwa adui zake mpaka msalabani. Nasi tumejitoa kabisa kwake, mwili na roho.

**20.** Para hii inaendelea kuzungumzia udogo unaotupasa, kwa kutumia manenoya Mt. Fransisko mwenyewe. Inachora sura tunayotarajiwu kuwa nayo zaidi na zaidi, kadiri ya maendeleo ya kiroho, sio tu kati yetu, bali hata ulimwenguni, tunapohusiana na watu wa kila aina. Ushuhuda huo unalenga amani, ambayo ni ukamilifu wa neema za Mungu. Ni kama kwamba tunasikia kwa ufupi mawaidha ambayo mzee wetu alikuwa akiwapa Ndugu zake alipowatuma kuhubiri kwa matendo na maneno. Kabla yake, ndivyo alivyofanya Yesu alipowatuma kwanza mitume halafu wanafunzi wengine sabini na wawili. Sawa na mwalimu wake, Mt. Fransisko alisisitiza namna ya kwenda kuliko maneno ya kusema.Kuna sifa tano ambazo zinatufaa hasa tukiwa kati ya watu ili kuwapa ushuhuda wa maisha ya Kiinjili hata kabla hatujasema neno. Baadhi ya sifa hizo ni kati ya heri alizotangaza Yesu, baadhi ni maadili ya kibinadamu na pia matunda ya Roho Mtakatifu. Hivyo tunaelekezwa njia ya ukamilifu aliyoipitia Mt. Fransisko hata akachuma matunda hayo na kuonja heri hizo.

**Ndugu wa kiume na wa kike wawe watulivu** Upole unaturithisha nchi, yaani miyo ya wenzentu. Kwa hiyo tuachane na uhasama, chuki, hasira, kelele, matusi ili kuwa na moyo mwema na wenyewe kuhurumia watu Kol.3 8, 12. Yesu aliwataka mitume wawe kama wanakondoo kati ya mbwamwitu. Utulivu uvute hata wapinzani kwenye mawazo ya amani.

**Wenye amani** Sifa ya kwanza imeshatuingiza katika hii ya pili ambayo pia ilitangazwa na Yesu kuwa ni heri. Ni Ndugu kuwa na amani rohoni hata kuieneza kwa watu, ndio wanaostahili kweli kuitwa wana wa Mungu. Juu yao Mt. Fransisko alisema, Wenye amani kweli ni wale ambaa katika yale yote wanayoyavumilia ulimwenguni humu, kwa upendo wa Bwana wetu Yesu Kristo, wanadumisha amani rohoni na mwilini mwao.

**Wataratibu** Sifa ya tatu ni ile ya wanaoratibu vilivyo mawazo, maneno na matendo yote hasa hamu ya ukoo na ya kudadisi na kuwa na adabu njema katika vitendo vya mwili, michezo na sura ya nje. Adili hilo la kibinadamu linamfanya mtu apendeze, jambo ambalo ni muhimu katika utume ili ujumbe usikataliwe kwa sababu ya tabia ya mjumbe. Tawi la kwanza la utaratibu ni unyenyekevu, ambao Mt. Fransisko aliutaja wazi mwishoni, baada ya upole, akikumbuka Yesu alivyojifanya kielelezo cha hayo mawili hasa Math.11 29.

**Wapole** Sifa ya nne inalingana na ya kwanza, isipokuwa kule ilikuwa ni heri, hapa ni adili linaloratibu ono la hasira ili litokee tu panapohitajika, kama lilivyomtokea Yesu Yoh.2 13 17 ingawa alikuwa havunji mwanzu uliopindika wala kuzima utambi ufukao moshi Math.12 20, sio lilivyowatoka mitume dhidi ya waliomletea watoto Math.19 13 14 na ya Wasamaria Lk. 9 54 55. Kwa namna ya pekee uzingatiwe mfano wake msalabani Lk.23, 34 43. Basi, Mfransisko apokee wote kama Yesu, na kupunguza ukali wa maonyo anayopaswa kuyatoa, tena pengine avumilie dhuluma na dharau za kila aina Math. 5, 39 41. Kwa kufanya hivyo Ndugu Wadogo wa kwanza waliwapata waliwakosea, hata baadhi yao wakaingia shirikani.

**Na wanyenyekevu** Sifa hiyo iantajwa mwisho, lakini si ya mwisho kwa umuhimu, bali pamoja na ufukara ndio msingi wa utawa wetu, tena kwa Wakristo wote ndio msingi wa maisha ya kiroho, kwa kuwa unaondoa kiburi ambacho ni mzizi wa vilema vyote na kizuo cha kujaliwa neema Yak.4 5. Ndiyo sababu unatajwa mara nyingi katika kanuni. Mt. Fransisko alihimiza Ndugu wote wenye kuhubiri au kusali au kufanya kazi, makleri kwa mabradha, wajinyenyekeshe katika yote, bila ya kujitokuza wala kufurahi kwa ndani wala kujipongeza moyoni kwa maneno au matendo mema au kwa mema yoyote ambayo Mungu anasema au kutenda au kufanya pengine kwa njia yao. Watambue kuwa mema yote ni ya Mungu tu, hivyo wamrudishie yeye, na kumshukuru kwa hayo, kwa kuwa yanatoka kwake, naye tu anastahili kupata sifa na ibada, heshima na utukufu na shukrani, kwa kuwa jema lolote ni la kwake yeye aliye mwema peke yake Mk. 10 18.

Kwa msingi huo Mt. Fransisko na wenzake walipendelea kudharauliwa kuliko kusifiwa, wakijua tusi linahimiza kujirekebisha, Kumbe sifa inaangusha kwa kuchochea kiburi. Vivyo hivyo walitanfaza makosa yao wenyewe na kukumbusha uwezekano wa kutenda maovu makubwa zaidi siku za mbele, na kwamba jambazi angepewa neema nyingi kama wao angeweza kuwa na shukrani zaidi kwa Mungu. Hatimaye walikuwa chini ya wote na kupendelea kazi duni zenye kuleta dharau Fulani.

**Wakiongea na wote kwa uadilifu inavyofaa** Maneno yalingane na maadili yao na kuyasaidia kuwajenga wasikilizaji, kwa kukwepa hasa uongo na mengine yote yasiyowafaa watakatifu Ef. 4 25 5 3.

**Basi, popote walipo au wanapokwenda ulimwenguni** Yaani utawani na kati ya watu wa kawaida, wakiwa na sifa hizo tano, wakwepe makosa matatu yafuatayo na kutokeza tena sifa nyingine maalumu.

**Wasigombane** Wala kati yao wala na watu wengine. Wakikumbuka hotuba ya mlimani wakwepe ugomvi hata kama unalenga kutetea haki zao au kudai fidia ya kosa walilotendewa. Kwa kujifanya wadogo na kujinyima haki hizo wanaweza kuyatekeleza maneno ya Injili kwa urahisi zaidi na hivyo kutosababisha kuta ambazo ziwatenganisha na Ndugu zao, kwa kuwa hata mdhulumaji ni mtoto wa Baba wa mbinguni au anaitwa awe hivyo.

**Wala wasishiriki katika mabishano** Hayo pia hayapatani na udogo, bali yanatokana na majivuno na nia ya kufanya mtazamo Fulani ushido mitazamo mingine, labda hata baada ya kuona ukweli ni tofauti, tena yanazuia mtu asiwaelewe wengine, na yanasaababisha mafarakano, dharau, makwazo n.k. Kumbe mtumishi wa Mungu alitabiriwa kuwa hatateta wala hatapaza sauti yake Math.12 19

**Wala wasiwalaumu wengine** Kwa mfano uliotolewa na Mt. Fransisko kwa msingi wa kuwa wanakula na kunywa vinono na wanavalia nguo maridadi, yaani hawaonyeshi toba kama ile ya Mfransisko. Anayehukumu anajipandisha juu ya wengine hata kushika nafasi ya Mungu Math. 7 1, hivyo hafuati udogo. Tena hajui kuwa anaowahukumu siku yoyote wanaweza wakabadilika kuwa waadilifu, basi ni afadhali kila mmoja ajilaumu na kuhidharau mwenyewe Kanuni ya Kudumu, 2 17.

**Bali wajionyeshe wafurahivu katika Bwana** Hakuna kanuni ya kitawa iliyowahi kuwa na agizo kama hilo, kabla Mt. Fransisko hajaandika ya kwake ya Muda 7 16. Maneno yenye kwa mtume Paulo Fil. 4 4 , lakini kimsingi ni onyo la Yesu dhidi ya unafiki wa wanaokunja nyuso zao ili kuonekana na watu kuwa wamefunga. Maisha ya Mfransisko ni magumu, lakini yeye ajaa furaha, hata kufurika yaani kuonekana. Furaha hiyo si ya kidunia, inayoendana na starehe, bali ni ya kidini, inatokana na imani, hivyo inatakiwa kudumu hata katika majaribu. Mt. Fransisko alijitahidi daima kuwa na furaha hiyo, inayokuwa kamili katika majaribu makali zaidi, kama la kudharauliwa na wafuasi wake mwenyewe na kuachwa na Mungu ilivyoonekana kwake. Alionya kwamba mtu asipoweza kujionyesha mfurahivu, au akitaka kulia machozi juu

ya ukosefu wake, abaki chumbani mwake hadi arudi katika hali ya kawaida.

**Na wachangamfu na wapendevu kiasi cha kufaa** Tabia hiyo ya Kikristo inatakiwa ujulikana na watu wote Fil.4 5. Upendevu ni adili mojawapo la kibinadamu alilokwanalo sana mzee wetu, na ni sehemu muhimu kwa karama yake iliyovuta na bado inavuta wote kwake. Katika utume tone la asali ni bora kuliko pipa la siki. Mradi tusipite kiasi cha kufaa. Tuwe tayari kutangaza ukweli hata ukichukiza wasikilizaji, tusipende kuridhisha daima watu, la sivyo hatuwezi kuwa watumishi wa Kristo, tukumbuke maneno mengine pia ya Mt. Fransisko alivyotoa ole wake kwa mtawa anayechekeshachechesha tu, tuangalie upendevu wetu usielekee upande wa mapenzi kwetu au kwa wenzetu.

**Halafu kusalimu wasalimu kwa kusema, Bwana akupe amani** Mt. Fransisko alikusudia kanuni yake iwe kama mkate mmoja uliotengenezwa kwa kuunganisha makombo ya Injili. Basi, si ajabu kwamba inatufundisha kusalimu kama Bwana alivyowafundisha Mitume, halafu mwenyewe kwa namna ya pekee. Mzee wetu, askari aliyegeuka kuwa mtu wa amani, alisisitiza hata kufa kwake Wasia 23 salamu ya Kiinjili, yaani kuwatachia watu amani kamili, ya kijamii na ya kiroho pia. Hapo kwanza, salamu hiyo ilishangaza sana, hata ilimbidi awahimiza Ndugu wasikate tamaa ya kuitumia. Baadaye watu wakaipenda na kuitamani.

### **SURA YA SITA MAISHA YA UFUKARA**

Sura hii inatufafanulia maisha ya ufukara kadiri ya Mt. Fransisko. Kumuongokea Mungu mfululizo maana yake kwake ni kufuata nyayo za Yesu. Kwamba tunawezeshwa kufanya hivyo, ni habari njema. Neno linatwaa mwili ndani mwetu kama ilivyokuwa ndani ya Yesu, yaani katika ufukara wa Kiinjili, wa roho na wa mali, wa ndani na wa kijamii.

Upande wa roho, ufukara ni kukiri unyonje wetu kwa moyo wote, tukikubali kuwa dhambi tu ni za kwetu, mema yote ni ya Mungu. Hata wokovu wetu unamtegemea yeze tu, kwa kuwa sisi hatuwezi kufanya lolote. Ufukara huo, uliosisitizwa hasa katika Mawaihda, unatuweka wazi kupokea neema za Bwana.

Upande wa mali, ufukara ndio hali inayothibitisha kuwa Mungu tu ni muhimu na inayotufanya tumtumainie yeze kwa yote tunayoyahitaji. Ufukara huo unatuunganisha na wapenzi wa Mungu waliotangazwa wenye heri kwa kuwa Mungu amewaandalia ufalme wake. Ndiyo habari njema aliyotangaza Yesu.

**21.** Para hii inatuletea mshono wa maneno ya Mt. Fransisko kuhusu sababu za kushika ufukara, pamoja na baadhi ya vipengele vya utekelezaji wake. Ufukara haufafanuliwi kinadharia, ila unaonyeshwa katika Bwana wetu Yesu Kristo, aliye njia yetu ya uzima. Yeye alijishusha kabisa ili kutuokoa na kutoonyesha ndani mwake namna ya kupokea huo wokovu wake. Tunapaswa kujishusha hata kimaisha, kwa kuridhika na viachache, kujihadhari na pesa, na kushikamana na fukara ili watukaribishe mbinguni.

**Ndugu wote wa kiume na wa kike wajitahidi kufuata unyenyekevtu na ufukara wa Bwana wetu Yesu Kristo** Kwa maneno hayo Mt. Fransisko anatushirikisha wito aliojaliwa kwa kuvutiwa hasa na sifa hizo mbili za Bwana, unyenyekevu na ufukara. Hizo zinahusiana sana, kiasi kwamba katika Biblia zinachanganyikana.

**Ambaye akiwa tajiri juu ya yote** Maneno ya 2Kor. 8 9 aliyoyatumia Mt. Fransisko kufafanulia ufukara, yametumika pia katika hati za Mtaguso Mkuu wa II wa Vatikano kama kielelezo cha ufukara wa watawa wowote.

**Hata hivyo aliamua, yeze pamoja na Bikira Mwenye Heri Mama yake** Ufukara wao ni wa hiari, yaani umechaguliwa makusudi kadiri ya matakwa ya Mungu. Ndiyo namna bora ya kuhusiana na mali ile ya Yesu na ya Bikira Maria. Mt. Fransisko aliuunganisha katika jambo hilo, akizingatia walivyoshiriki hali moja toka mwanzo. Akikumbuka ugumu wa maisha yao, mzee wetu alikuwa anatoka machozi mengi.

**Kujichagulia ufukara ulimwenguni** Ni chaguo la Kimungu, ni namna ya Kimungu ya kuishi ulimwenguni, hivyo inatufaa tumfuate.

**Akajishusha kabisa** Maneno hayo ya Fil. 2 7 yana uzito wa pekee katika Kigiriki, kiasi kwamba si rahisi kuyatafsiri. Ni kuachana na hali ya asili ili kuitwaa nyingine duni kabisa, isiyolingana nayo. Wafransisko wanavutiwa na fumbo hilo kwa namna ya pekee, walizingatia katika sala na katika maisha, kujishusha kabisa kwa mfano wa Mwana wa Mungu

**Basi, wakumbuke ya kuwa hakuna kitu ambacho ni lazima tuwe macho katika ulimwengu wote**  
Maneno hayo ya Kanuni ya Muda 9 1 yanasisitiza kuwa mahitaji ya kweli si mengi, ila tamaa hazina mwisho. Ulimwengu umejaa vitu vinavyotuvutia, lakini tusidanganywe na tamaa, vya lazima ni vichache. Tuisahau ukweli huu tunapofikiria kujipatia kitu ambacho kwanza hatukuwa nacho. Tuliweza kuishi bila ya hicho, na wengi wanaishi vilevile bila ya hicho.

**Isipokuwa kwamba, tukiwa na chakula na nguo, tunaridhika navyo, kama Mtume alivyosema.**  
Ni swala la kuridhika na maisha, la sivyo tutazidi kuhangainia vitu, badala ya kumtamani Mungu tu. Ukwelie huo wa 1Tim. 6 8 unawafaa watu wote, lakini Fansisko aliupigia mstari kwetu, kama siri ya kiroho, kama njia maalum ya wokovu. Ufukara mkuu aliotufundisha unaanza na vitu, unaendelea na mapendo ya kibinadamu hata ukashinda kabisa, kwa kutoshikamana na matakwa yetu, wadhifa au utume Fulani n.k.

**Tena wajihadhari sana na pesa** Onyo hilo la Mt. Fransisko Kanuni ya Muda 8 11 lilikazwa zaidi katika Kanuni ya Kudumu likawa katazo kali la matumizi yoyote ya pesa. Utawa wa Tatu unapokea onyo, ila si katazo. Kwa vyoyoyote tuelewe sababu zake za kuchukia pesa aliyoita mavi ya shetani, nzi, nyoka mwenye sumu, mavumbi ya njiani na kwa majina mengine ya dhara. Akiwa mtoto wa mfanyakia tajiri alitambua wazi jinsi hela zinavyoweza kutawala moyo wa binadamu wenyewe umimi, hata azitumikie badala ya Mungu Lk. 16 13. Pesa zinaweza yote kwa kuwa zinanunua yoyote, hata mwili na roho vya watu. Vipande vichache vinaweza kumwasha mtu tamaa kubwa ajabu na kumnyanganya tunu zote, kama vile haki, urafiki, shukrani kwa mwingine na kwa Mungu, iliyomtokea Yuda, Mt. Fransisko aliposhika ufukara alifurahia wepesi wa hali hiyo iliyomlinganisha na ndege wa angani wasio na ghala, wanaolishwa na Mungu mkarimu siku kwa siku. Hasa hakusahau kwamba Yesu aliwakataza mitume wake wasichukue hata pesa chache katika safari yao ya kwanza aliowatuma kuhubiri. Jambo hilo hatuwezi kulipuzia, kama kwamba kwetu hakana shida yoyote.

**Halafu wanapaswa kufurahi wanapishi kati ya watu duni na wanaodharauliwa, kati ya fukara na dhaifu na wagonjwa na wakoma na wanaoombaomba njiani** Ndio wenzetu, ndio watu ambaa Mungu anawapendelea, ndio walengwa wakuu wa habari njema, ndio watu ambaa Mt. Fransisko alitamani kushiriki kabisa hali yao kwa kushuka tabaka, ndio watu ambaa watawa wowote wanapaswa kuwapenda kwa tumbo la Kristo, uliyosema Mtaguso, ndio watu ambaa kuwapenda kweli ni dalili ya uteule. Tutahukumiwa juu ya uhusiano wetu nao, kwa kuwa ni Yesu hai kati yetu. Tunapaswa kujisikia raha ya kuwa nao, kuliko kuwa na wenyewe uwezo. Hao ndio walimu wetu wanaotufundisha mengi kuhusu ukweli wa maisha. Ni maneno ya Kanuni ya Muda 9 2.

**22.** Para hii ni mshono wa maneno ya Mt. Fransisko kuhusu ufukara mkuu, hasa kutoka Kanuni ya Kudumu, sura ya 6, ambayo ndio kiini cha kanuni nzima, ambapo mzee wetu anatufungulia moyo ake bila ya kubanwa na wanasheria. Nusu yake ya kanza inawakataza Ndugu Wadogo wasimiliki chochote, wala binafsi wala kijumuia. Kama tulivoona katika para ya 21, ye ye alijua kuwa binadamu hawezu kuishi asipotumia walau vichache, ila alitofautisha kumiliki na kutumia. Aliwaruhusu wafuasi wake watumie vitu kifukara, mradi visiwe vya kwao, yaani wavitumie kama kwa kuazima, bila ya kuweza kudai haki yoyote juu ya hivyo, hata waweze kunyanganywa bila ya kupinga kwa maneno au kwa silaha au kwa kukimbilia mahakama. Hivyo alielekeza uhuru wa moyo usiohangainia chochote isipokuwa kumpendeza Mungu.

**Wale walio maskini wa roho kweli, kufuatana na mfano wa Bwana** Yesu ndiye kielelezo cha ufukara wa Kiinjili, unaohusu roho na vitu.

**Hawajitwalii chochote wala hawashindani na mtu kwa hicho** Maneno hayo ya Kanuni ya Muda 7 13 yanatukumbusha Mt. Fransisko aliyohama Rivotoro asije akashindana na mkulima aliyeingiza punda katika nyumba ya kitawa. Ndivyo aliyofundisha Bwana Yesu katika hotuba ya mlimani, kujinyima haki ili kudumisha amani ya moyoni na amani na watu. Ndio msimamo ambaa tuwe nao, ingawa kanuni yetu haitamki katazo la kumiliki kisheria.

**Bali wanaishi ulimwenguni humu kama wasafiri na wageni** Maneno hayo ya 1Pet. 2 1 yalimgusa sana Mt. Fransisko hata akayaandika na kuyatamka mara nyingi. Anayesafiri kwa miguu hasa hawezu kubeba vingi. Ingawa tunaelekeea kutia mizizi tunapoishi, Mt. Fransisko alisifu Luchido aliyekuwa tayari daima kuhama asishikamane na mahali popote.

**Hiki ndicho kilele kirefu cha ufukara mkuu** Kanuni yetu, ingawa haikupokea katazo la pesa na la kumiliki kisheria, wala himizo la kuombaomba, inatuelekeza kwenye kilele cha ufukara mkuu. Faida zake zinakuja kuelezwaa mara moja.

**Unaotufanya sisi warithi na wafalme wa utawala wa mbinguni** Kwa kuwa bibi ufukara aliolewa na

Bwana akatuzaa kwa sura yake. Na Yesu mwenyewe aliahidi ufalme wa Mungu kwa fukara.

**Umetufanya maskini katika vitu, watukufu katika maadili** Maneno hayo ya Mt. Fransisko yanafuata yale ya Yak. 2 5. Ni kwamba ufukara unastawisha unyenyekevu, unazoesha kufanya malipizi, unakinga na uzinifu, unatutia huruma kwa wenye shida, unalisha tumaini, unaimatisha utiifu n.k.

**Ufukara huo uwe ndio fungu letu** Ndio sehemu bora tuliyopangiwa na Mungu, kwa mfano wa Walawi ambaa Bwana alikuwa ndiye fungu lao, na ndiye sababu hawakugawiwa nchi ya Israel. Tufurahie urithi wetu huo.

Kwa kuwa unatuongoza kwenye nchi ya walio hai Yaani kwenye uzima wa kweli. Kwa kuachana na dunia hii, tunazidi kutumainia na kusogelea mbingu.

**Hata tukishikamana nao kabisa** Kwa moyo wote kama na mpenzi.

**Kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo tusitake kitu kingine chochote kuwa nacho daima chini ya mbingu.** Tutumie chochote kwa muda tu, bila ya kufungamana nacho moja kwa moja. Tufanye hivyo kwa ajili ya Yesu, fukara hata leo katika wadogo wake.

### **SURA YA SABA MAISHA YA UDUGU**

Baada ya ufukara mkuu, unaotuingiza katika mashaka mengi, Mt. Fransisko na vilevike kanuni yetu alizungumzia upendo wa kidugu ambaa tuwe nao. Ni kwa sababu ugumu wa maisha yasiyo na tegemeo la kibinadamu unatakiwa kutuunganisha zaidi kati yetu. Katika shida zetu sisi maskini wa Mungu tunaweza kukimbilia hasa jumuia yetu, tukijua Ndugu zetu wa kiroho wanatupenda, hivyo watafanya juu chini ili kutusaidia.

Upendo huo ni wa kidugu, msingi wake ukiwa ni uhusiano wetu na kaka Yesu na umoja wa wito tuliojaliwa kwa kumfuata yeye. Kama upendo wa Ndugu wa jamaa moja, ule wa Wafransisko unatakiwa kujotokeza kwa urahisi kama ule kati ya wenye damu moja. Mafungamano kati yetu, tena na viumbe vyote, yawe ya namna hiyo na kutekelezwa vizuri Kimungu na kibinadamu. Kwetu jamaa ni familia, sio tu jumuia ambapo tunachanga baadhi ya mambo sala, utume, mali n.k.

Kwa msingi huo, sura hii inatukumbusha wajibu wa kupendana kama Yesu alivyotupenda, kwa kusisitiza upande wa wagonjwa na wakosefu. Aliyepatwa na udhaifu wa mwili au wa roho, anahitaji zaidi kupendwa na kusaidiwa.

**23.** Para hii inatushonea maneno ya Biblia na ya Kanuni za Mt. Fransisko ili kuweka msingi wa upendo ndani ya Mungu na kutuelekeza kuutekeleza katika shida halisi za maisha ya kila siku.

**Ndugu wa kiume na wa kike wapendane kwa upendo wa Mungu** Ndilo neno zito zaidi aliloweza kutumia Mt. Fransisko na alilojali kuliko yote. Upendo wa Mungu. Hata kabla ya kuongoka hakumkatalia mtu aliyemuomba kwa ajili ya upendo wa Mungu.

**Kama Bwana alivyosema, Hii ndiyo amri yangu, mpendane kama nilivywapenda ninyi** Mzee wetu alitumia maneno hayo ya Yoh. 15 12 ili kusisitiza haja ya kupendana na namna ya kupendana, yaani bila ya mipaka, kama Yesu alivyofanya kwa ajili yetu hadi msalabani. Mengine mengi ni mashauri, hiyo ni amri.

**Basi, waonyeshe kwa matendo upendo walio nao wao kwa wao** Hapa mkazo wa Mt. Fransisko maneno yaliyotangulia na hayo yamo katika Kanuni ya Muda 11 5 6 ni upande wa utekelezaji. Kama kawaida yake, hakuridhika na maneno mazuri, bali alidai matendo kulinana na 1Yak. 2 18 na Yoh. 3 18.

**Basi, watoleane shida zao bila ya shaka, ili kutafutiana na kusaidiana wanayoyahitaji** Kutokana na udugu, mwenye shida asione shaka kuieleza kwa mwenzake yeyote, na hasa kwa wahudumu. Lakini hata kabla ya hapo mwenye upendo wa kimama aweze kutambua shida hizo na kujitolea kadiri ya uwezo wake. Hivyo ufukara mkuu hauwezi kutisha.

**Wana Heri wale wanaompenda mwenzao akiwa mgonjwa, wakati asipoweza kuwasaidia, sawa na anapokuwa na afya na uwezo wa kuwasaidia** Ndio ujumbe wa Mawaidha 24. Upendo si wa kujitafutia faida. Na mtu hathaminiki kwa kuzingatia anaweza kutupatia nini. Mt. Fransisko ndiye kielelezo

cha upendo huo. Yeye aliongoka kwa kumhurumia mgonjwa wa ukoma, akawa na huruma kubwa ajabu kwa wagonjwa wote, hata akasahau maradhi mengi tena makubwa aliyokuwa nayo. Hasa kwa wanajumuia wenzake alijua kuwa ufukara mkuu ni mgumu kwa mzima, lakini ni mgumu zaidi kwa mgonjwa anayehitaji vitu nya pekee matibabu, vyakula vinono n.k. Kwa hiyo aliwakumbusha Ndugu wazima kanuni ya dhahabu Math. 7 12. Hasa wajibu huo mzito ni wa wahudumu, ingawa wanaweza kuutekeleza kwa njia ya wengine ambao wahakikishe mgonjwa asikose mahitaji yake ya kiroho na ya kimwili. Tukipaswa kuwasaidia wowote wenye shida, kwa namna ya pekee tunapswa kuwasaidia Ndugu zetu wanaotutegemea moja kwa moja sisi wanajamaa. Ni haki yao tuwasaidie hata kwa kuacha shughuli nyininge. Ushuhuda huo wa udugu ni muhimu kuliko mahubiri yenewe. Tusijisingzie kuwa tunahitajiwa na watu wa nje hata kuwaacha Ndugu zetu wa kiroho katika ugonjwa na ufukara pasipo msaada.

**Halafu wamshukuru Muumba kwa yote yanayowatukia, tena watamani kuwa anavyowataka Bwana, ama wazima ama wagonjwa** Tujiachie mikononi mwa Mungu moja kwa moja, tukijua anatunyosha hasa kama anatupenda zaidi ili tuingie katika uzima wa milele Mdo. 13 48, Ufu. 3 19. Baada ya ujumbe huo, katika Kanuni ya Muda 10 3, Mt. Fransisko ametuachia lawama kali kwa wale wanaohangaikia mno afya na kusumbua wenzao kwa kudai matibabu. Halafu katika Kanuni ya Kudumu 10 9 akatushauri tutamani kuliko yote kuvumilia ugonjwa pamoja na mengineyo. Kwa sababu hiyo katika ugonjwa tujiachie mikononi mwa Mungu na mwa wenzetu, tukipokea kwa mikono miwili yale tunayopewa, tukikumbuka kuwa fukara wengi wanayakosa hata hayo.

Ikiwa wanashirika wengine kwa busara na upendo watamsaidia mgonjwa asijisikie ametengwa wala kusahauliwa na jumuia, naye atabeba msalaba wake kwa manufaa ya wote, kuanzia jumuia yenewe, maradhi yataujenga sana kama nafasi maalumu ya kumpendeza Mungu na kushikamana wenewe kwa wenewe kwa upendo na uvumilivu.

**24.** Tunaishi duniani bado. Para hii inatukumbusha ukweli huo kwa kutuelekeza kuhusu ukosefu wetu unaoathiri maisha yetu ya kiroho na ya kijumuia. Msamaha na huruma ndizo dawa zinazotufaa.

**Ikija kutokea kwa neno au ishara sababu ya vurugu kati yao** Umoja wetu unaweza ukavurugwa hata na neo au ishara moja isiyofaa.

**Mara moja, kabla ya kutoa mbele ya Mungu sadaka ya sala yake** Ni muhimu kuwahi kabla mambo hayajaharibika zaidi. Mtakatifu Klara anatuambia tuwahi kabla ya kumtolea Mungu sala, ambayo ni sadaka mojawapo Math. 5 24, la sivyo sala itashindikana kwa kukosa amani moyoni.

**Mmoja amuombe kwa unyenyekevu mwenzake amsamehe** Msamaha unatekeleza upendo na kujenga jumuia. Si rahisi kuishi bila kukoseana. Mradi tuwe na unyenyekevu wa kuomba msamaha na upendo wa kutoa kila mara. Math. 18 35.

**Ikiwa mmojawapo amevunja vibaya mtindo wa maisha aliotamka ahadi ya kuushika** Hapa linazungumziwa jambo lingine, si tena makosa madogomadogo kati yetu, bali dhambi kubwa dhidi ya ahadi yetu ya kitawa. Kanuni inadai tufuate utaratibu wa Injili wa kumkosoa kidugu aliyefanya hivyo. Mt. Fransisko alidai tuwe na hisani kwako kama kwa mgonjwa, hata dhambi ikiwa kubwa namna gani. Ndio moyo wa Injili nzima. Mtu wa Kiinjili anapaswa kuwatendea wakosefu kama Yesu alivyofanya, akitufunulia sifa bora ya Mwenyezi Mungu, yaani huruma. Hapo awali Mt. Fransisko alidai Ndugu aliyezini avuliwe kanzu na kufukuzwa shirikani. Lakini alipoendelea kiroho akaona wazi ubora wa huruma akadai watumishi wawe wakali kwa wazushi tu.

**Aonywe na mtumishi au na wengine waliopata kujua kosa lake** Upendo wa kidugu unatudai hivyo. Hasa mtumishi aliyekabidhiwa Ndugu anapaswa kukosoa.

**Nao wasisababishe apatwe na aibu, au kupotewa na sifa njema, bali wawe na huruma nyangi kwake.** Maneno hayo Mt. Fransisko alimwandikia mtumishi Fulani 15. Barua hiyo inaonyesha alivyoshinda mafadhaiko kwa kasoro za shirika lake akimuachia Mungu yote hata akakabili ukosefu wa Ndugu zake kwa dawa iliyo bora na kuhimiza wote wafanye vilevile kulingana na Injili, kwa kuwa sio wazima wanaohitaji daktari, bali walio wagonjwa Math. 9 12.

Katika hamu yake ya kuokoa Ndugu wote aliokabidhiwa, alipowaachia watumishi madaraka yake alitamka hadharani, watakiwe kujieleza kwako Bwana siku ya hukumu, ikiwa Ndugu yeoyote atapotea kwa ulegevu wao au kwa mfano wao mbaya au kwa ukali unaopita kiasi. Maandishi yake yanafundisha kumsaidia mkosefu ajirekeshe. Kwanza kwa kumtegemeza asije akaanguka tena na kwa kumtia moyo aamini uwezekano wa kushinda dhambi. Halafu kwa kumuonya, kumfundisha na kumkosoa. Mwishowe kwa kufidia yaliyomshinda,

Nasi tukiona au kusikia kuwa Mungu anachukizwa....basi, tumtukuze na kumsifu. Kila dhambi inapunguza moto wa upendo ulimwenguni, lakini tukimchukia aliyeitenda tunaupunguza zaidi. Kumbe tukiwajibika kwa upendo kufidia hasara hiyo, uadilifu wa Ndugu mmoja unashinda hata wingi mkubwa wa watu dhaifu, kama vile mwali mmoja wa nuru unavyoondo magiza makuu.

Badala ya kudai wote wawe wakamilifu tayari, kutumia huruma pamoja na juhudi motomoto kunajenga kweli jamaa. Ndiyo kazi ya kila siku, ndiyo neema ya kuiomba kila siku, na hapo katikati ni pia msalaba wa kuubeba kila siku. Utawa ni njia ya ukamilifu ambayo tunaifuata kwa kuwa hatujafikia mwisho wa safari sisi wala Ndugu zetu. Katika njia hiyo huruma ina nafasi muhimu kwa sababu inatuletea huruma ya Mungu, anayewaonea huruma daima Ndugu zake hayuko mbali na utakatifu.

**Lakini wote wanatakiwa kuepuka kwa uangalifu wasikasirikie dhambi ya mtu yeote au kuchukizwa nayo, kwa kuwa hasira na kinyongo vinazuia upendo wao na wa wengine.** Ndiyo maneno ya mwisho ya sura ya 7 ya Kanuni ya Kudumu. Tunapaswa kuangalia maitikio yetu yatokane na upendo tu na kuuchangia. Hasira na kinyongo havifai, bali wema na upole. Mwenye huruma kwa mfano wa Baba wa mbinguni ameahidiwa na Yesu kuwa ataonja heri.

### **SURA YA NANE UTIIFU WENYE UPENDO**

Kwa kawaida utiifu, unaozungumziwa katika sura hii, unahusishwa na imani, kwa kuwa undai tukubali maongozi ya Mungu asiyonekana. Kumbe kichwa cha sura katika kanuni yetu kinatumia neno maalumu la Mt. Fransisko, Utiifu wenyе upendo. Kwake utiifu unahusiana na upendo na kujenga jumuia badala ya kuivuruga kwa umimi. Kulingana na msimamo wake, kanuni inasisitiza utiifu, lakini bila ya kusahau kwamba wahudumu pia wanapaswa kumtii Mungu kwa njia ya kanuni na amri ya upendo pamoja na kuheshimu dhamiri za Ndugu zao. Kwa kuwa lengo la cheo chao ni kuisaidia jumuia iitikie wito wake kwa umoja, na kila Ndugu aifuate sauti ya Mungu anayoisikia rohoni mwake. Basi wahudumu wasiwe mabwana bali watumishi wa wenzao, na hao wa pili wawatii kabisa kwa upendo.

**25.** Para hii, ikitumia maneno mbalimbali ya Mt. Fransisko katika Kanuni ya Muda na ile ya Kudumu, inasisitiza utiifu wa Yesu Kristo. Yeye hasa ni Mwana wa Baba, na kwa hiyo alijali kumtii kuliko yote. Sisi tunaomfuata na kutaka tuwe kweli wana wa Mungu, tunapaswa kumtii vilevile. Wahudumu na Ndugu wengine wote wayatamani matakwa ya Mungu kuliko chakula, wafadhaike kama mimi mpaka waweze kunywea kikombe kichungu cha utiifu hata kufa msalabani. Hivyo tu watakuwa tayari kujikana na kujikatalia matakwa yao, katika kujifanya watumishi tu wenyе kuwaosha miguu wenzao, au katika kuwatii wenyе mamlaka kama Yesu alivyowatii wazee wake.

Bwana Yesu alifundisha kuwaheshimu wenyе mamlaka kwa kuwa hiyo inatokana na Mungu Yoh. 19.11, na alithibitisha amri ya nne ya Mungu kwa watu wote Mk.7 9 - 13. Hivyo utiifu ni wa lazima katika kuishi na watu katika familia, jamii na Kanisa. Zaidi ya hayo watawa wanajifunga kwa namna ya pekee kumtii Papakama mkuu wa mashirika yote na kuwatii wanashirika wenzao walioshirikishwa mamlaka ya Kanisa katika ngazi mbalimbali ili kustawisha jamaa yao.

**Kwa mfano wa Bwana Yesu aliyweweka matakwa yake katika matakwa ya Baba.** Mara nyingi tunapenda kumvuta Mungu alingane na matakwa yetu, Kumbe tunapaswa kujilinganisha na ya kwake, kama Yesu alivyofanya na alivyofundisha. Utakalo lifanyike.

**Ndugu wa kiume na wa kike wakumbuke ya kuwa wamekana matakwa yao kwa ajili ya Mungu.** Utiifu kwa Mt. Fransisko unafanana na kukamilisha ufukara, Akifanua Lk. 9 24 na 14 33 katika Mawaihda aliandika, Mwenye kuachilia kila kitu alichonacho na kupoteza mwili wake ndiye yule ajitoaye mhanga kwa utiifu mikononi mwa mtumishi wake. Ni kilele cha ufukara, kwa kuwa ni kujinyima kilicho bora, yaani si vitu tu, bali matakwa yetu. Lakini ni rahisi kusahau kwamba tumemtolea Mungu sadaka hiyo.

Hivyo kanuni, kabla haijasisitiza mengine, inawakumbusha wote wajibu huo wa moja kwa moja. Kama vile maisha yote ya Yesu, ya kwao pia yaongozwe na kuanganishwa na lengo moja, Tazama nimekuja, ee Bwana,. Niyafanye mapenzi yako Eb. 10 5 - 10. Sadaka hiyo ni kwa ajili ya Mungu, yaani inatolewa kwa roho ya imani na upendo kwa matakwa ya Mungu, unavyoeleza Mtaguso. Sadaka hiyo inamuabudu kuliko nyingine, kwa kuheshimu ukuu wake na mamlaka yake juu ya maisha yetu yote, si juu ya mambo kadhaa tu. Halafu inaunganisha kwa imara na hakika zaidi na matakwa ya Mungu, yaani na mpango wake wa kuwaokoa watu. Tukitii mfululizo tunamuabudu mfululizo na kuchangia mfululizo wokovu wa watu, tena vizuri kuliko kwa kujipangia sala au utume Fulani. Pengine utiifu unamurai mtu afe kama chombe ya ngano, yaani aweke pembeni au kumwaga kabisa mambo bora aliyonayo k.mf. vipawa, hapo akumbuke sheria ya \injili ya kufa ili

kufufuka, kuoza ili kuzaa sana. Anayetaka kuahidi utiifu awe na imani imara katika sheria hiyo na awe tayari kuishika kweli bila ya kujijali.

Utiifu haumhusu tu binadamu anayeagiza, bali Mungu aliyempa mamlaka ili akikuagiza umsikilize kwa niaba yake. Ndiyo sababu haifai kuzingatia binadamu huyo ni nani, au anafanya kazi yake vipi, wala maagizo yake kama yanafaa au sivyo. Mt. Fransisko alionya kwamba aliye chini hatakiwi kumuona binadamu tu katika mkubwa wake, bali Yule ambaye kwa ajili yake anamtii. Akakiri kwamba kati ya neema alizonijalia Bwana, mojawapo ni ile ya kuwa tayari kumtii mara mnovisi wa mwisho ambaye ningepewa kama mlinzi, sawa na kumtii Ndugu mzee na mwenye busara kuliko wote.

Ni kwamba imani inaona yote kwa undani kabisa, kwa macho ya Mungu, si juujuu kama binadamu, kwa mfano inamuabudu Yesu katika ekaristi, bila ya kuzingatia padri yupi amefanaya mageuzo, na mkate upi umetumika. Basi, anayetuagiza kwa niaba ya Mungu tunapaswa kumtii hata kama ni mtu duni asiyefaa, na hata kama agizo lake linaonekana la kipumbavu, kumtii Mungu katika nafasi ya namna hiyo kunampendeza kwa namna ya pekee na kulipwa naye kuliko tukitii kwa kumpenda kiongozi au kupendezwa na agizo lake kutaka kusifiwa naye.

**Katika mikutano yote wanayofanya** Jamii yoyote ya binadamu duniani inahitaji miundo ya kufaa ili istawi na kufanya kazi vizuri. Familia, chama, nchi, Kanisa na vinginevyo vina miundo tofauti kulingana na mtindo wake, mazingira yake, lengo lake n.k. Tena miundo hiyo inarekebishiwa mara kwa mara kusudi izidi kufaa. Mt. Fransisko alipaswa kubuni miundo mipy kwa utawa wake wa aina mpya. Alifanya hivyo kwa kupitia mangamuzi mbalimbali na kwa kusaidiwa na viongozi wa Kanisa, wataalamu wa sheria na Ndugu zake, hata akafaulu kulinda hali ya kifamilia na usawa kati ya wote.

Muundo wa kwanza kuzungumziwa na kanuni yetu ni mikutano ya ngazi mbalimbali. Wamonaki pia walikuwa na muundo huo toka zamani, lakini kwa Wafransisko una sura mpya kwa sababu zifuatazo, hakuna abati yaani baba wa wamonaki anayetawala mkutano, bali wote ni Ndugu tu, wenyewe haki sawa ya kusema na kuamua, katika mkutano mkuu na mkutano wa kanda wajumbe hawatoki nyumba moja, bali mazingira mbalimbali, hivi kwamba inatawala furaha ya kuonana na kupashana habari baada ya siku nyingi, kutokana na mangamuzi yao kuwa tofauti, hata mitazamo na matazamio vinaweza vikawa tofauti sana na kufanya mkutano kuwa wa fujofujo, kwa vyovytote hali ni ya kifamilia, haibani sana na taratibu zilizopangwa

**Watafute kwanza ufalme wa Mungu na uadilifu wake.** Kadiri ya Math. 6 33, mengine yote watapewa kwa ziada. Tofauti na mashirika mengi, ambapo maswala ya uchumi yanahitaji kujadiliwa sana, Kanuni ya Muda inatamka wazi kuwa mikutano inakusudiwa kujadili mambo yanayomhusu Mungu, yaani kwanza maisha ya kiroho, halafu malezi uongozi n.k. 18 1.

**Na kuhimizana ili waweze kushika vizuri zaidi kanuni waliyoahidi na kufuata kwa uaminifu nyayo za Bwana wetu Yesu Kristo.** Utekelezaji wa kanuni ndiyo njia ya kufuata nyayo za Yesu katika utawa wetu, kadiri tulivyoahidi.

**Wasitawale wala kutumia mabavu hasa kati yao.** Maneno hayo na yafuatayo yametoka katika Kanuni ya Muda 5 9, 14 15, na kusindikizana na maneno mbalimbali ya Injili kuhusu udogo na utumishi Math. 20 25, Lk. 22 26. Mtindo wa uongozi katika Ukristo na hasa katika Ufransisko unatakiwa kuwa tofauti sana na ule wa siasa. Kwa sababu hiyo Mt. Fransisko hakukubali majina ya ukubwa waliyoyazoea watawa, bali alitumia tu majina yanayopatikana katika Agano Jipy, mtumishi na mtumwa Math. 20 24 28, mtunzaji na mlinzi Yoh. 10 3, 1Pet.2 25, hayo yote yanasisitiza upendo kuliko mamlaka.

**Kwa upendo wa roho watumikiane na kutiiana kwa hiari.** Ndiyo Mt. Fransisko alivyopanua maneno ya Gal.5.13. Kwake kutii ni swala la upendo, hivyo tukipendana, tunapaswa kutumikiana na kutiiana hata tusipobanwa na ahadi. Ndivyo udogo unavyoleta picha ya utamaduni wa upendo unaokusudiwa ulimwenguni kote.

**Basi, huo ndio utiifu halisi tena mtakatifu wa Bwana wetu Yesu Kristo.** Kwa mara nyingine Mt. Fransisko anaweka mbele yetu kielelezo cha utiifu ambacho tukifuate.

**26.** Para hii fupi inatokana na Kanuni ya Kudumu 8.1 na kuzungumzia wadhifa wa juu unaouunganisha Ndugu wote walioawanyika ulimwenguni, na upana wa utiifu wa Kifransisko.

**Wapaswe daima kuwa na mmojawao kama mtumishi mwenye kuhudumia jamaa.** Yaani kila shirika liwe na mkuu wake, mmoja kwa wanashirika wote duniani. Kwa mtazamo wa Mt. Fransisko, huyo ni Ndugu tu mmojawapo aliyepewa kazi ya kuosha miguu ya Ndugu zake kama alivyofanya Yesu. Shirika

halitakiwi kubaki bila ya mtumishi wa namna hiyo kwa kufa, kujiuzulu au kumaliza muda, hivyo badala ya mmoja achaguliwe mwingine.

**Ambaye wapaswe kabisa kumtii katika yale yote waliyomuahidia Bwana kuyashika na ambayo hayapingani na roho na kanuni hii.** Katika mashirika mengi utiifu unahusu tu maisha ya kijumuia na utume wake kadiri ya katiba. Kumbe kwa Wafransisko utiifu ni mpana iwezekanavyo, kwa sababu wanaruhusiwa kukataa maagizo yale tu ambayo ni dhambi. Mt. Fransisko akitaka ukamilifu wa hali ya juu katika kila jambo ametudai tujikane kabisa kwa kujikatalia matakwa yetu yote. Alisema, Najua tunda la utiifu, na kwamba hakuna nukta isiyoleta faida kwa mtu aliyeinama ili kuongozwa na mwingine. Mtiifu ana amani na furaha moyoni, amejikomboa na kupata nguvu rohoni. Kwa msingi huo Mtaguso wa II wa Vatikano unawataka watawa watumie nafsi yao yote, uwezo wa akili na utashi, na pia vipaji vya neema na vya maumbile katika kutekeleza maagizo na katika kuwajibika na wadhifa wao. Wafanye vizuri iwezekanavyo kwa kuwa wanamfanya Nungu.

Wasia 27 30 unatuhimiza kumtii kiongozi kama watumwa wasioweza kwenda wala kufanya lolote mbali na matakwa ya bwana wao. Mt. Fransisko aliwahi kutoa mfano mwingine, umchukue maiti na kumweka unakotaka, ukimuondoa hapingi, ukimlaza halalamiki, ukimuangusha hadi kitu, ukimtawaza anaangalia chini tu, ukimvika nguo ya zambarau anaonyesha zaidi rangi ya mfu usoni. Ndivylo aliyo mtiifu wa kweli, haulizi kwa nini ameondolewa, ahangaiki kuhusu mahali popote anapowekwa, hanganganii kuhamishwa, akipandishwa cheo anazidi kuwa mnyenyeketu, akiheshimiwa zaidi anazidi kujiona hafai.

Mifano hiyo isieleweke vibaya kama kwamba mtawa asitakiwe kuwajibika kadiri ya uwezo wake, akichunguza hali halisi ili kuona inafaa afanye nini. Wala usieleweke kama kwamba mtawa asubiri tu kuagizwa, bila ya kumsaidia mhudumu wake kwa kumpa maoni aliyonayo. Kadiri ya Mtaguso, watawa watii kwa uvumbuzi na kwa kuchukua majukumu ya matendo yao watii kama wana wa Mungu waliokombolewa kutoka hofu, watii kama watu waliokomaa nafsini mwao. Watu wa namna hiyo, kwa ustawi wa jumuia katika amani, na kwa imani katika mpango wa Mungu aliyempa mamlaka mhudumu wao, baada ya kueleza maoni yao, wako tayari kufanya tofauti, tena bila ya kununua wala kulalamika, wakitulia katika matakwa ya Mungu ambayo kwa hakika ni bora kuliko ya kwao, ingawa hayaonekani kuwa hivyo mara moja.

Tukiachiwa nafasi ya kuamua wenyewe, tukumbuke maneno ya Mt. Fransisko, Na lolote atendalo na kusema, ambalo anajua si kinyume cha mapenzi mhudumu wake, ni utiifu wa kweli, mradi lile atendalo ni jambo jema. Kwetu si muhimu agizo litolewe wazi ili tutii, bali tuchunguze daima mhudumu anataka tufanya nini hata kabla hajanena, kusudi tuwahi kutekeleza. Tukizoea hivyo, kwetu itakuwa rahisi kumtii mara na kwa furaha akituagiza, kwa sababu maneno ya mhudumu hayaji kuvuruga mipango yetu, bali yanatusaidia tutambue wazi matakwa yake yanayofafanua yale ya Mungu, mradi yasiende kinyume cha dhamiri yetu na cha kanuni tuliyomuahidia Mungu palipo dhambi hapana utii.

**27.** Para hii inatuochorea utekelezaji wa uhusiano unaotakiwa kati ya watumishi na watawa wao. Ingawa wanaishi mbali, kuna haja ya kukutana mtumishi awatembelee watu wake, nao wamkimbilie katika shida za kiroho hasa. Karibu maneno haya yote yanatokana na Kanuni ya Kudumu 10 3 6.

**Wale walio watumishi wenye kuwahudumia wengine.** Ndio mkazo wa Mt. Fransisko kuhusu namna ya kuongoza, ni utumishi tu, kadiri ya Injili. Isiwe hivyo kinadharia tu jina mtumishi lilingane na msimamo na mwenendo.

**Wawatemelee.** Njia ya kwanza inayowezesha kutumikia ni ziara, kwa mfano wa Bikira Maria kumtembelea Elizabeti ili kumtumikia katika uja uzito, bila ya kujali mimba yake mwenyewe iliyomfanya Mama wa Bwana. Kutokana na upendo, alifunga safari kwa haraka aliposikia tu shida ya Ndugu yake. Ikawa furaha kubwa kwa wote.

Kuanzia Mtaguso wa IV wa Laterano hadi leo Kanisa linadai viongozi wote wa watawa wawatemelee ili kuwakinga na upotovu, kuondoa maovu, kutatua matatizo, kukosoa na kuhimiza jumuia nzima na kila mmoja binafsi. Sababu ni kwamba kila mwenye madaraka juu ya wengine anapaswa kujitahidi afahamu hali yao ili awshughulikie vizuri. Hivyo wakikaa mbali awatembelee kadiri ya uwezo wake.

Mbali ya ziara ya kidugu, ambayo haina masharti maalumu, sheria zina agiza ziara rasmi za mara kwa mara, na kuziwekea malengo na masharti. Kila Ndugu atoe mchango wake ili kuzifanikisha, akijibu kwa ukweli na upendo maswali yoyote ili mgeni aelewé hali halisi aweze kuchukua hatua za kufaa. Kwa kawaida kabla ya ziara kila Ndugu awakosoe wenzake kidugu Math.18 15 17. Upande wake mtumishi asisau masharti mengine ya Injili yanayotajwa na kanuni mara moja.

**Na kuwaonya na kuwfariji kwa unyenyekevu na upendo.** Maadili hayo mawili yatafanya ziara isifanane na upelelezi wa kipolisi, bali iwe na ile sura ya kifamilia inayosaidia zaidi kujenga jamaa. Mtumishi asisahau lengo hilo, anapotumia njia mbili tofauti, kuonya na kufariji. Watu wanazihitaji zote mbili, mara hii, mara hii, au zaidi hii kuliko hii.

**Basi, Ndugu wa kieme na wa kike ambao wanajua na kufahamu ya kuwa hawawezi kuishika kanuni jinsi ya kiroho. Tukizingatia** Kanuni ya Muda sura ya 5 tunaelewa maana ya neno hilo la mwisho, yaani kwamba Mt. Fransisko alitaka kutofautisha mwenendo wa Ndugu wanaoongzwa na Roho Mtakatifu katika kushika kanuni sawasawa, na mwenendo wa wale wanaoishika ili mradi, wakifuata zaidi matakwa ya mwili yanayopingana na yale ya Roho. Hakuwa na maana ya kupuuzia maneno yenewe ya kanuni ili kujidai kufuata roho yake tu. Bali alisitiza mpaka kufa Wasia 38 39 kanuni ishikwe bila ya kuongeza wala kupunguza neno, wala kuitia maelezo yasiyolingana na unyofu na usafi wake.

Basi, Ndugu akiona kwamba mazingira fulani yanazuia asishike kanuni vilivyo, jinsi Roho anavyomsukuma kufanya, asiogope kuwajibika kwa kumueleza mtumishi wake.

**Popote walipo wana wajibu na ruhusa ya kuwakimbilia watumishi wao. Jambo** hilo la pekee ni sababu mojawapo ya urawa wa Kifransisko kukosa utulivu katika historia yake na kuota matawi mapya yenye kufuata urekebisheso. Mt. Fransisko alitabiri hayo yote pamoja na kwamba shirika litalegea hata kuwatesa wenye nia njema kama hiyo. Ndiyo sababu aliweka wazi kuwa ni haki kumtii Mungu kuliko binadamu, yaani dhamiri kuliko mwenendo wa jumuia. Kwa kusema wenye moyo wa kufuata kanuni vizuri kuliko shirika kwa jumla linavyofanya wana wajibu na ruhusa ya kujieleza tena wanatakiwa kusikilizwa sana, Mt. Fransisko alisababisha kwa makusudi shirika karibu kila wakati liwe na Ndugu wenye bidii na nia ya kushika kanuni Kiroho. Baadhi yao waliruhusiwana watumishi waunde nyumba maalumu ambamo sala na ufukara vizingatiwe zaidi, baadhi ya waliokataliwa walifikia hatua ya kujitenga na uongozi rasmi wa shirika. Mara nyingi matawi hayo mapya yalikubaliwa na Kanisa yakazaa matunda mengi ajabu ya utakatifu na utume, yakithibitisha hivyo asili yao ya Kimungu.

Ni kwamba Mfransisko, sawa na watawa wowote, anapaswa kutoa ushuhuda wa kijumuia, hata katika ufukara. Tena akikumbuka sifa yake ya kwanza ni udugu, anahitaji ushirikiano mkubwa zaidi na wenzake. Basi, kama hakuna maelewano juu ya ufukara hasa, anajisikia kutoweza kutekeleza wito wake, mpaka jumuia nzima iwe na msimamo mmoja.

Mbali ya Ndugu wanaosongwa hivyo na dhamiri zao, haki na wajiby wa kumkimbilia mtumishi ni wa wale wote wanaoshindwa kutimiza kanuni sawasawa, mradi yawepo masharti matatu kwanza, Ndugu awe anazuiwa sana hata kuwa kweli katika hatari ya kuvunja ahadi na kutenda dhambi, pili, asimkimbilia mtumishi kwa kufadhaishwa na saikolojia yake tu, bali kutokana na hali halisi, tatu, awe anazuiwa na mazingira, yaani hatari isitokane na uovu wake mwenyewe la sivyo ajirekebishe tu.

**Upande wao watumishi wawapokee kwa upendo na wema.** Ndilo agaizo la Mt. Fransisko ambalo mara nyingi halikutekelezwa, kwa sababu watumishi walijiona na mamlaka ya kuamua lolote, bila ya kuzingatia kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya wenzao. Wahudumu wanapaswa kuwajibika kwa niaba ya Mungu na kadiri ya mapenzi yake kwa ajili ya afya ya mwili na roho ya Ndugu zao, mmojammoja na katika jumuia. Kuoanisha yote kunawadai busara kubwa na hasa kipaji cha shauri. Wakiwa nacho hawatapinga kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya wenzao.

Ili kuepusha ulegavi shirikani, wao wachochee hamu ya ukamilifu na kulisha maisha ya kiroho ya jumuia, hivi kwamba kila Ndugu awajibike asihitaji kusukumwasukumwa. Pia wayaunde mazingira yawe tayari kuupokea uvuvio wa Roho Mtakatifu, hasa unapowatia Ndugu kadhaa nia ya kushika vizuri zaidi kanuni. Nia hiyo ni utajiri mkubwa kwa shirika zima unaolihimiza kufuata juhudhi na mifano yao bora, hivi kwamba ulegevu unaepukika au kufidiwa.

Kinyume chake anatenda mtumishi yule ambaye bila ya sababu anakataza au kuzuia matendo ya hiari ya toba kwa kisingizio cha kwamba, eti hataki ndugu ajitokeze kufanya vizuri kuliko wenzake. Msimamo huo unazimisha kazi ya Roho Mtakatifu na kuleta uvuguvugu katika jumuia. Kwa sababu mtu hawezি kufikia utakatifu akifuata tu matendo ya wengi, kwa kuwa hao wengi si watakatifu hata wakijitahidi, tena hawezی kutimiza vizuri wajibu wake asipotenda kwa hiari mambo kadhaa yasiyompasa kisheria, na hasa asipoitikia mialiko ya Roho anayemuongoza kwa ndani.

**Na kutimiza udugu wao kwo** Mamlaka haiondoi udugu, nbali inadai utimizwe na watumishi kwanza.

**Hata wale waweze kuongea nao na kuwatendea kama vile mabwana wanavyowatendea**

**watumwa wao.** Yaani kwa kuona walivyokaribishwa vizuri, watawa wajisikie kweli mabwana wa watumishi wao. Na hao wakubali kuambiwa na kutendewa kama watumishi wa watumwa wanavyofanyiwa na mabwana zao.

**Kwa kuwa ni lazima iwe hivyo kwamba watumishi wawatumikie kweli wote.** Ndiyo sababu wanaitwa hivyo. Kwa mara nyininge tunaona unyofu wa Mt. Fransisko, hakutaka watumishi libaki kuwa jina lisilo na maana halisi. Alichagua jina hilo liwe kweli na maana ya kutumikia. Likumbushe lazima hiyo.

**28.** Para hii fupi kuliko zote inatuangalisha tusishikilie nafasi za uongozi, bali tuwe tayari kuwaachia wengine, kwa kuwa huduma ni za muda. Wazo linatokana na Kanuni ya Muda 17.4, ambapo Mt. Fransisko alisema kuhusu kazi za mtumishi na mhubiri. Kushikamana nazo ni kinyume cha ufukara mkuu. Hizo si mali yetu, ila tunakabidhiwa, hivyo tunaweza tukaondolewa pia.

**Basi yeьте asijitwalie huduma Fulani.** Maidha 4.3 yafananisha tendo hilo na lile la Yuda aliyejitwalia mfuko aliokabidhiwa. Kumbe mtumishi aone kazi yake kuwa kama ile ya kuosha miguu ya wenzake, yaani asiitamani. Hapo ataweza kuwa tayari kuiacha bila ya mshtuko.

**Bali wakati uliopangwa ukifika.** Kulingana na sheria za Kanisa kwa watawa, uongozi unatakiwa kupangiwa muda maalumu isipokuwa kwa mashirika machache, mkuu anaweza kuwa wa kudumu. Mtu akizoea kutawala, anaingia hatari nyding za kiroho, mojawapo ikiwa ni kiburi. Pia badiliko linaweza likaleta mawazo mapya yanayohitajika na bidii mpya ili kukabili hali mpya ili kukabili hali mpya na kutoridhika na ile iliyopo.

**Aache kazi yake kwa moyo radhi.** Bila ya kujiona mnyonge na kulalamikia wenzake, eti hawana shukrani, au hawaoni ubora wake. Kwa kweli kuacha nafasi ya juu kwa moyo radhi ni dalili kubwa ya maendeleo ya roho.

#### **SURA YA TISA MAISHA YA KITUME**

Baada ya kufafanua ushuhuda wa maisha ya Kiinjili katika udogo, ufukara na udugu, pamoja na msingi wa wito wetu, mzizi wake katika sala na uhusiano kati yetu, sura ya mwisho ya kanuni inakabili swala la utendaji ambao kwa kila shirika unategemea jinsi lenyewe lilivyo kwa ndani, yaani katika uhusiano wake na Mungu kuititia mafumbo maalumu ya Kristo, na pia katika uhusiano na watu.Uamuzi wetu wa kujitoa kabisa kwa Mungu ili tudumu katika upendo wake, hauwezi kubaki bila ya matokeo kwa watu wengine. Kwa njia yetu upendo wa Mungu unawafikia wengine. Utendaji wenyewe ultazamwa na Mt. Fransisko kama uenezi wa sala. Hivyo sura hii ni kilele cha zile zilizotangulia, hasa inapotukumbusha tunapaswa kuwa tayari kuuawa kwa jili ya Kristo.

Hata ndani ya Ufransisko, kila shirika linatakiwa kuwa na lengo na mbinu maalumu katika utume. Kwa Utawa wa Kwanza ni hasa huduma ya Neno la Mungu kwa waamini na wasioamini. Kwa Utawa wa Pili nia maombezi tu. Kwa Wasekulari wa Utawa wa Tatu ni kuumua malimwengu kutoka ndani yake. Kwa mashirika ya Utawa wa Tatu, kanuni haisemi wazi lengo ni lipi, kwa kuwa yako mengi sana hivyo katiba zitaeleza kinaganaga, ila kwa wote kanuni inaonyesha roho ya Kifransisko katika utume

**29.** Para hii inaanza na maneno ya kwanza ya Himizo kwa Ndugu wa Toba.Ni kwamba msingi wa maisha ya kitume ni upendo kwa Mungu na kwa jirani. Bila ya upendo tunapiga kelele na kuhangaika tu, tusiweze kufanikisha chochote. Maneno yanayofuata yametwaliwa katika katika Barua kwa Shirika lote 8 9 ili kutukumbusha kwamba tumetumwa ulimwenguni ili kmshuhudia Bwana.

**Ndugu wa kiume na wa kike wampende Bwana kwa moyo wote, kwa roho na akili yote, kwa nguvu zote.**Mzee wetu alitumia;dondoo hilo. Mk. 12 30 alipotaka kueleza toba ni nini, kwamba ni kumuongokea Mungu kabisa kwa upendo kuliko kutenda mambo fulanifulani sala, sadaka, mfungo n.k. Pasipo upendo hayo hayafai. Ni vilevile kuhusu matendo ya utume yasipotokana na upendo kwa Mungu, hayafai. Ndiyo sababu tunapaswa daima kuhakikisha uwiano mzuri kati ya maisha ya kiroho na maisha ya kitume, kwa mfano wa Yesu na wa Mt. Fransisko. Ni lazima utume utokane na maisha ya sala hasa, ili tushirikishe yale tuliyoyachota katika kuongea na Mungu na kuzama katika mafumbo ya imani tunayotaka kushuhudia. Uwiano mzuri wa sala na utume ni tunda linaloiva tu baada ya kulilenga kwa bidii muda mrefu.

**Na kuwapenda majirani wao kama nafsi zao wenyewe.** Ni wazi kwamab utume unadai vilevile upendo kwa majirani, hasa kuwatokia yaliyo bora kabisa, yaani uzima wa milele. Upendo huo udhihirike katika maneno na matendo yetu yote.

**Nao wamtukuze Bwana kwa matendo yao.** Mt. Fransisko alitumia dondoo hilo la Tob. 13.6 linaloonyesha kwamba tunapaswa kumtukuza Mungu kwanza kwa matendo kuliko kwa maneno tu. Ndio mkazo wa mzee wetu, ushuhuda wa maisha kabla ya tangazo wazi la Habari Njema

**Kwa kuwa aliwatuma ulimwenguni kote.** Ndio mtazamo wa kimisionari wa Yesu amba Mt. Fransisko aliufufua zamani zake. Wafuasi wake wajisikie wametumwa, hivyo lazima waende, si katika nchi moja au chache, labda zile za jirani au rahisi zaidi, bali kokote. Kweli mpaka leo Wafransisko wametekeleza sana neno hilo katika mabara yote, wakichangia kwa iasi kikubwa uenezaji wa Iinjili duniani, bila ya kuzuiwa na ugumu wa safari, hatari za kuuawa, matatizo ya mazingira n.k. Muhimu ni kwamba tumetumwa.

**Kusudi waishuhudie sauti yake kwa kusema na kutenda.** Kadiri nafasi inapoturuhusu, tunapaswa pia kumshuhudia Yesu kwa midomo yetu, tikitangaza jina lake ambalo peke yake linaleta wokovu.

**Nao wawajulishe wote ya kuwa yeye tu ni Mwenyezi.** Maneno hayo pia yametoka katika Tob. 13.4. Kama vile Wayahudi walijiona wametawanya katika ya mataifa yote ili kumshuhudia \mungu kuwa ndiye peke yake Mungu hai na wa kweli, sisi pia tunapaswa kufanya hivyo mbele ya watu wowote, wanaozidi kuiabudu miungu ya bandia, kuanzia pesa.

**30.** Para hii inaeleza tabia ya utume wa Kifransisko amani, upole, hisani na utayari kwa kudhulumiwa. Tumetumwa kama kondoo kati ya mbwamwitu, kadiri Yesu alivyosema na Mt. Fransisko alivyokumbusha.

**Kwa vile wanatangaza amani kwa sauti, wawe nayo kwa wingi zaidi moyoni mwao.** Kwa mara nyingine **tunaangalishwa** tusiridhike na maneno mazuri. Amani ifurike kutoka ndani ya miyo yetu. Hivyo tu maneno yetu yataeneza kweli amani ya Kristo. Tudumishe amani moyoni hata katika nafasi ngumu namna gani.

**Mtu yeyote asibabaishwe nao kupatwa na hasira au kikwazo.** Mt. Fransisko alichukia jambo hilo kiasi kwamba alitoa laana kwa wafuasi wake watakaotoa kikwazo kwa wengine, wakiwafanya wasiamini au wasifuate maadili.

**Bali wote wavutiwe na upole wao kwenye amani, wema na uelewano.** Kama alivyofanya mzee wetu, aliyefaulu kupatanisha hata miji mizima. Inatosha tukumbuke alivyopatanisha Askofu na Meya wa Asizi kwa kuwaimbia Utensi wa Ndugu Jua alipokuwa mahututi

**Kwa kuwa Ndugu wa kiume na wa kike wameitwa kwa ajili hii, ili watibu waliojeruhiwa, wawafunge jeraha waliovunjika na kuwarudisha waliopotea.** Yaani wawe Wasamaria Wema kwa yeyote mwenye shida. Maneno hayo mazuri yametwaliwa katika Ngano za Wenzi Watatu 58, ni dondoo pekee la kanuni lisilotokana na maneno ya Mt. Fransisko mwenyewe. Limepitishwa kwa sababu linachora vizuri moyo unaotakiwa kutusukuma tuwahudumie wenzetu kiroho na kimwili.

**Halafu popote walipo wakumbuke ya kuwa wamejitoa na kuacha miili yao kwa Bwana wetu Yesu Kristo.** Tumejitoa kwake mwili na roho, kama yeye alivyofanya hata msalabani. Hivyo tuwe tayari kushiriki kifo chake, bila ya kukwepa hatari. Baada ya ushuhuda wa maisha na tangazo wazi la Injili, ushuhuda wa damu ndiyo njia ya mwisho ya kushughulikia wokovu wa watu. Ndio ushuhuda mkuu wa ukweli tuliofunuliwa na wa upendo unaotusukuma.

**Basi, kwa upendo wake wanatakiwa kujitolea kwa maadui wanaonekana na wasioonekana.** Kama Yesu alivyojitoa kwa waliokuja kumkamata. Hakuondolewa uhai, bali aliutoa mwenyewe. Tusiogope wanaoweza kuua mwili wetu tu. Tueneze imani, tutetee haki na kufanya yote yanayotupasa bila ya kukwamishwa na hofu. Maneno haya, pamoja na yale yanayotangulia na yanayofuata yametokana na sura ya 16 10 12 ya Kanuni ya Muda, sura ya pekee katika kanuni zozote za kitawa, kwa sababu ndiyo ya kwanza kuzungumzia wazi utume kwa Waislamu na kwa wengine wasio Wkristo, ambao hasa wakati huo ulikuwa hatari.

Ndiyo sababu Mt. Fransisko alipenda kukabili mwenyewe kazi na hatari za namana hiyo, akituonyesha tunavyopaswa kujitolea kwa maadui kwa ajili ya Kristo. Wafuasi wake wengi wakafuata mfano wake wakamfia Yesu kwa furaha.

**Kwa sababu Bwana anasema Wenye heri wanaoudhiwa kwa ajili ya haki, kwa kuwa ufalme wa mbinguni ni wao.** Ndiyo kilele cha heri nane ambazo Yesu alizitangaza mlimani kama katiba ya ufalme wa Mungu. Kama kawaida, Mt. Fransisko anatuelekeza juu, katika ukamilifu wa Kiinjili ambapo tunawenza kuonja heri ya kweli hata katika mateso.

**31.** Para hii inaeleza kwamba tunaweza kuchangia utume kwa namna mbalimbali, lakini tukiri kuwa mema yote yametoka kwa Mungu, sio kwetu. Hivyo tumtukuze yeze badala ya kujitokuza wenyewe kwa mema anayoyafanya ndani mwetu na kwa njia yetu. Mawazo hayo yametwaliwa katika Kanuni ya Muda 17 5 6, 17.

**Katika upendo ambao ni Mungu.** Daima Mt. Fransisko alikubali maombi aliyoelekezewa kwa upendo wa Mungu Mbele ya upendo huo usio na mipaka, aliona hawezi kumkatalia mtu chochote kile. Naye mwenyewe alipotaka kusitiza ombi lake alitumia usemi huo. Ila aliubadilisha kidogo kwa kuzingatia maneno ya 1Yoh. 4 16, kwamba Mungu ni upendo wenyewe.

**Ndugu wote wa kiame na wa kike, wawe wanásali au kutumikia au kufanya kazi.** Ndiyo baadhi ya tofauti kati ya Wafransisko. Mzee wetu alitanguliza wale wanaohubiri, akaongeza makleri kwa mbaradha. Wote kwa jumla wanaweza kuchangia utume wetu, kila mmoja kadiri alivyojaliwa na Mungu, kwanza wanaoshika maisha ya sala tu, halafu wanaotoa huduma mbalimbali za kiroho na za mwili, hatimaye wanaofanya kazi kwa mahitaji ya jumuia. Katika nafasi hizo na nyinezo wasisahau lengo la kitume kwa kumtolea Mungu wanachofanya ili ufalme wake ufike

**Wajitahidi kujinyenyekeza katika yote.** Yaani kukiri ukweli ya kwamba mema yote ni ya Mungu, na ubaya ni wa kwetu. Wajikumbushe daima kuwa ndivyo ilivyo, wasijitwalie yaliyo ya Mungu kama kwamba ni ya kwao. Sisi ni maskini kweli mbele yake. Afadhali tukubali.

**Kutojituza wala kutojipongeza wala kutojikuza kwa ndani.** Pengine aibu inatuzuia tusijipongeze kwa nje, lakini hiyo haitoshi. Mt. Fransisko anatuhimiza tusijikuze hata kimawazo, la sivyo tunamuibia Mungu utukufu wake.

**Kutokana na maneno na matendo mema au kwa jema lolote ambalo pengine Mungu anafanya au kusema au kutenda ndani yao au kwa njia yao.** Baada ya maneno hayo Mt. Fransisko alitaja yale ya Yesu kwa mitume waliporudi washindi juu ya mashetani Lk. 10,20. Mafanikio si muhimu kwetu. Tunaweza kufkuza mashetani na kufanya miujiza tusimpendeze Mungu Math. 7,21 23. Unyenyekevu tu utatuwezesha kushika nafasi yetu, ile ya vyombo duni vya uweza na wema wa Mungu. Kadiri tunavyomnyenyekeea ndivyo kadiri ya ukweli, ndivyo atakavyotutumia kwa mafanikio makubwa zaidi.

**Kila mahali na katika nafasi yoyote watambue ya kuwa mema yote ni ya Bwana Mungu Mkuu na mtawala vyote.** Kumbe, alivyo sema Mt. Fransisko, tujuu kwa hakika kwamba hakuna cha kwetu isipokuwa vilema na dhambi zetu.

**Nao wamtolee shukrani yeze ambaye mema yote yanatoka kwake.** Mt. Fransisko alipokea kwa moyo wote himizo la mtume Paulo la kuwa na shukrani. Kumshukuru Mungu kwa yote, ndio wajibu wetu hata kwa mema anayotenda kwa wengine kutupitia sisi. Tumshukuru kwa kututumia katika kusababisha mema, badala ya kujitokuza kama kwamba tumetenda mema wenyewe.

## **HIMIZO NA BARAKA**

**32.** Para ya mwisho ya kanuni inatuletea mambo mawili, himizo na baraka. Yote mawili yanalenga kutuchochea tuwe waaminifu kwa neema tuliyojaliwa na Mwenyezi Mungu. Yote mawili yanatumia maneno ya Mt. Fransisko. Himizo ni mshono wa sentensi mbili muhimu za Kanuni ya Kudumu 10,8 na 12,4. Baraka ndiyo maneno ya mwisho ya Wasia aliotuachia mzee wetu akikaribia kifo chake kitukufu 40 41.

**Ndugu wote wa kiame na wa kike wazingatie ya kuwa ni lazima watamani kuliko yote.** Mt. Fransisko alionyesha mambo gani ni ya kuthaminiwa na ya kutamaniwa kweli, badala ya elimu iliyowavuta wengi, ikihatarisha udogo wa shirika lake. Aliorodhesha kupata Roho wa Bwana na kazi yake takatifu, kumuabudu daima kwa moyo safi, kuwa wanyenyekevu na wavumilivu katika dhuluma an ugonjwa, na kuwapenda wanaotudhulumu na kutulaumu na kutugombeza. Hayo yote yanategemea la kwanza, linalotajwa wazi katika kanuni yetu pia. Katika ufukara wetu mkuu tusitmani lingine kuliko hilo ambalo pekee linaleta uzima. Ni rahisi binadamu aishie katika mambo yanayoonekana kuwa na elimu, kuunda shule, kujenga kanisa kupata watu n.k. Kumbe yote ni bure kabisa yasipofanywa kwa Roho Mtakatifu, Bwana mleta uzima. Pasipo yeze, hata mambo matakatifu hayafai kitu, kusanyiko la waamini linabaki kundi la watu wasioelewana na wenye kugombania vyeo, Injili inabaki herufi tu, na utangazaji wake unabaki maneno matupu yasiyobadili maisha ya msikilizaji. Katika Kanuni ya Muda, Mt. Fransisko alimtaja mara 18, akiamini kuwa ndiye mhudumu mkuu halisi wa utawa na anafundisha waamini bila ya ubaguzi kati ya msomi na Ndugu myofu.

**Wawe na Roho wa Bwana.** Ndivyo mzee wetu alivyopenda kumuita Roho Mtakatifu, akifuata muelekeo wa mtume Paulo wa kusisitiza kwamba Roho anayemiminwa miyoni mwetu ni Yuleyule aliyuemuongoza Bwana Yesu. Ndiyo sababu huyo Roho anatutia hamu ya kumfuata Mwana wa Mungu kwa utukufu wa Baba, sio kujua na kusema maneno mazuri bila ya kuyatekeleza wenyewe, wala kuwa na dini ya kuonekana na watu ili kusifiwa nao Math. 6 2. Kadiri ya Mt. Fransisko, Roho wa Bwana anataka mwili ufishwe na kudharauliwa, kutothaminiwa na kupuuza, analenga unyenyekevu na uvumilivu, amani safi, sahihi na halisi ya roho, na juu ya yote anatamani uchaji wa Mungu, hekima ya Mungu na upendo wa Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Kanuni ya Muda 17 11 16.

**Na kazi yake Takatifu.** Maisha ya kiroho yanalenga kumuachia nafasi Roho Mtakatifu afanye kazi mwenyewe ndani mwetu na kwa njia yetu, kuanzia maisha ya sala. Mzee wetu aliogopa sana kumzimisha huyo Roho ndani mwake na katika shirika lake, kwa kupanga yote hata Roho asiweze kuvuma anakotaka. Alitaka tuwe wazi kabisa kwake kila anapotaka kutufanya kazi na jinsi anavyotaka kutufanya kazi. Kazi yake tu ni takatifu, si ile tunayoifanya sisi kwa kufuata roho yetu ya kibinadamu umimi au roho ya shetani, hata tukijipangia kazi za kitume. Ili asimzimishe Roho, Mt. Fransisko alikubali shirika lipatwe na vurugu katika historia yake. Pamoja na hayo, matunda yameiva kwa wingi.

**Halafu, wakikaa daima chini ya Kanisa takatifu.** Kanuni yetu, kama ile ya Ndugu Wadogo, inamalizika kwa kusisitiza tena yaleyale ya wanzoni, yaani maisha ya Kiinjili katika ufukara na unyenyekevu chini ya Kanisa Katoliki. Ndiko tunakoelekezwa na Roho Mtakatifu. Lengo la kuifuata Injili ya Yesu halipingani na himizo la kumtamani Roho kuliko yote. Hayo mawili yanaendana kama Yesu na Roho Mtakatifu. Yesu anaitwa Kristo kwa kuwa alitungwa, akapakwa, akaimarishwa mpaka kufa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, naye Roho ni zawadi ya Yesu aliyeemtoa aukamilishe ukombozi wake. Hatuwezi kumfuata Yesu pasipo nguvu ya Roho Mtakatifu, wala hatuwezi kudai tunamfuata Roho tukimpuzia Kristo na kukataa Kanisa lake. Hatushiki Injili tusipoishi katika Roho Mtakatifu, wala hatuishi katika Roho tusiposhika Injili, hasa amri kuu ya upendo.

**Na kuwa imara katika imani katoliki.** Bila ya msimamo katika imani sahihi, hatufiki popote, ila tunapepefushwa tun na udanganyifu wa watu Ef. 4 14 kadiri ya mitindo ya utamaduni wa ulimwengu usiohuishwa na Roho wa Bwana. Imani ndijo chanzo, mzizi na msingi wa wokovu, nayo inatufanya tuheshimu mamlaka ya viongozi wa Kanisa kama alivyofanya mzee wetu.

**Wafuate ufukara na unyenyekevu na Injili Takatifu ya Bwana wetu Yesu Kristo.** Yaani waishi kama alivyoishi yeye katika ufukara na unyenyekevu, kadiri inavyoolezwa na Injili yake. Sio tu kufuata mafundisho yake, bali nyayo zake.

**Walivyoahidi moja kwa moja.** Ahadi ni deni. Tumeitoa kwa moyo wote, sasa tuitekeleze mpaka mwisho wa maisha yetu na kwa neema yake hata kilele cha ukamilifu wa Kiinjili. Moja ka moja, bila ya kuangalia nyuma kwa yale tulio acha kwa ajili yake, ambayo tulijaliwa kutambua ni takataka mavi tu, yakilinganishwa na uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu. Fil. 3 7 14.

**Basi, yeьте atakayeyashika hayo mbinguni ajae baraka aliyejuu kabisa.** Ndiye asili ya baraka zote. Ndiye Mungu Mkuu, alivyopenda kumuita Mt. Fransisko. Kutoka juu kabisa aliko alitubariki kwa kuwatuma Mwana na Roho Mtakatifu duniani.

**Na duniani ajae baraka ya Mwanae na Roho Mfariji Mtakatifu sana.** Mt. Fransisko alipenda vilevile kuzingatia uhusiano wa Baba na Mwana, uliojumlishwa katika neno mpenzi, na uhusiano wa Roho Mtakatifu sisi, ulio jumlishwa katika neno Mfariji.

**Na malaika wote wa mbinguni.** Ambao Mt. Fransisko aliwaheshimu sana, hasa Mikael, na ambao walimfariji katika nafasi ngumu kabisa kwa utamu wa nyimbo zao.

**Na Watakatifu pia.** Tuwe na hakika ya kuwa wenzenzu hao wanatuombea, hasa Mama yetu Bikira Maria tuliyekabidhiwa kwake.

**Nami Ndugu Fransisko niliye mdogo sana, mtumishi wenu.** Ndiyo picha yake aliyotuachia, ile ya Ndugu mdogo, tena mtumishi wetu. Tukimfuata katika kujishusha mpaka mwisho, tutakwezwa juu kabisa kama yeye, ndani ya Utatu ulioteka roho yake.

**Kadiri ya uwezo wangu mdogo nawaimarishia kwa ndani na kwa nje baraka hiyo takatifu sana.** Mt. Fransisko alipokaribia kifo alizidi kubariki watu wowote aliohusiana nao, akaongeza na wale watakaoukuja nyuma kujiunga na shirika, akisikitika tu kwa kushindwa kuwabariki kulikouwezo wake. Baraka hiyo inafunga

kanuni yetu kwa kutuchochea tuanze kumtumikia Bwana Mungu kadiri ya para zake zote. Baraka hiyo ilikuwepo hata katika kanuni ya TOR ya mwaka 1927, hivyo inaunganisha Utawa wa leo na karne zilizotangulia kwa tumaini la kwamba sisi tutaweza kushiriki baraka hiyo waliyofurahia Ndugu zetu wote walioshika kanuni iliyo kitabu cha uzima, tumaini la wokovu, kiini cha Injili, njia ya ukamilifu, ufunguo wa paradiso, sharti la agano la milele, alivyosema Mt. Fransisko mbarikiwa.